

Ellen G. White Estate
KUMJUA
YESU
ELLEN G. WHITE

# KUMJUA YESU

**Ellen G. White**

**Copyright © 2021**
**Ellen G. White Estate, Inc.**

# Information about this Book

## Overview

This eBook is provided by the Ellen G. White Estate. It is included in the larger free Online Books collection on the Ellen G. White Estate Web site.

## About the Author

Ellen G. White (1827-1915) is considered the most widely translated American author, her works having been published in more than 160 languages. She wrote more than 100,000 pages on a wide variety of spiritual and practical topics. Guided by the Holy Spirit, she exalted Jesus and pointed to the Scriptures as the basis of one's faith.

## Further Links

A Brief Biography of Ellen G. White
About the Ellen G. White Estate

## End User License Agreement

The viewing, printing or downloading of this book grants you only a limited, nonexclusive and nontransferable license for use solely by you for your own personal use. This license does not permit republication, distribution, assignment, sublicense, sale, preparation of derivative works, or other use. Any unauthorized use of this book terminates the license granted hereby. (See EGW Writings End User License Agreement.)

## Further Information

For more information about the author, publishers, or how you can support this service, please contact the Ellen G. White Estate

at mail@whiteestate.org. We are thankful for your interest and feedback and wish you God's blessing as you read.

# YALIYOMO

# Contents

Information about this Book . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . i
YALIYOMO . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . iv
Sura 1—Jinsi Mungu Anavyowapenda Wanadamu . . . . . . . . . . . . . 6
Sura 2—Jinsi Mwenye Dhambi Anavyomhitaji Kristo . . . . . . . 12
Sura 3—Kutubu . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 16
Sura 4—Kuungama Dhambi . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 25
Sura 5—Kujitoa Kuwa wa Mungu . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 29
Sura 6—Kumwamini Mungu na Kukubaliwa Naye . . . . . . . . . 33
KUMJUA YESU . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 38
Sura 7—Dalili ya Kuwa Wanafunzi wa Kristo . . . . . . . . . . . . . . 39
Sura 8—Kukua Katika Kristo na Kuwa Watu Wake Wakamilifu 46
KUMJUA YESU . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 52
Sura 9—Kazi na Maisha, Jinsi Vinavyohusiana . . . . . . . . . . . . . 53
Sura 10—Kumjua Mungu . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 57
Sura 11—Kuomba ni Faradhi Yetu . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 62
Sura 12—Yatupasayo Kufanya Tukiwa na Mashaka Moyoni . . 69
Sura 13—Kufurahia Mungu . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 75

## Sura 1—Jinsi Mungu Anavyowapenda Wanadamu

VIUMBE vya ulimwengu, na jinsi Mungu alivyowafunulia wanadamu mambo yajayo, vyote huonyesha upendo wa Mungu. Baba yetu aliye mbinguni ndiye asili ya uhai, hekima, na furaha. Vitazame viumbe vyote jinsi vilivyo vizuri na vya ajabu. Fikiri jinsi vifaavyo kwa mahitaji na furaha, siyo ya wanadamu tu, bali ya viumbe vyote vilivyo hai. Jua na mvua, vinavyofurahisha na kuburudisha nchi, pamoja na vilima, bahari na mabonde, vyote hutuonyesha upendo wa Muumba wetu. Mungu ndiye anayeviruzuku viumbe vyake vyote mahitaji yao ya kila siku. Katika maneno mazuri ya Mtunga Zaburi twasoma haya,—

> “Macho yao wote yakutazamia wewe;
> Nawe huwapa chakula chao majira yake.
> Hufunua mkono wako,
> Humshibisha kila hai uradhi.”
>
> Zaburi 145:15, 16.

Mungu alimwumba mwanadamu katika hali ya furaha na utakatifu kamili; na wakati nchi ilipotoka mkononi mwa Muumba, ilikuwa
[8] nzuri kabisa; haikuwa na dalili ya uharibifu wala ya laana ya Mungu. Taabu na mauti viliingia kwa ajili ya kuharibu amri za Mungu. Walakini upendo wa Mungu huonyeshwa hata kwa maumivu yaliyokuja kwa ajili ya dhambi. Imeandikwa kwamba Mungu aliilaani ardhi kwa ajili ya mwanadamu. Mwanzo 3:17. Miti yenye miiba na magugu—yaani shida na majaribu yanayompata mwanadamu katika uzima wake—yaliwekwa kuwa msaada wake, kuwa ni namna mojawapo ya mafundisho yake yanayotakiwa katika mpango wa Mungu juu ya mwanadamu, ili apate kumtoa katika hali mbaya ya dhambi na kumrudisha katika hali njema jinsi alivyokuwa mara ya kwanza.

Ingawa dunia imeanguka katika hali mbaya kwa ajili ya dhambi, lakini yote yaliyomo si huzuni na mashaka. Viumbe vimekuwa kama

mitume wa Mungu kutuletea maneno ya kututia faraja na kututuliza roho zetu. Kila mti wa miiba una maua yake; yaani, katika kila shida twaweza kupata baraka za Mungu.

"Mungu ni pendo" imeandikwa kila mahali. Ndege waimbao vizuri, kila aina ya maua na miti,—yote hutushuhudia upendo na uangalifu wa Mungu, jinsi atakavyo kuwafurahisha watoto wake.

Neno la Mungu huonyesha tabia zake. Yeye mwenyewe ametangaza upendo wake na huruma yake visivyo na kiasi. Musa
alipoomba, "Nionyeshe basi utukufu wako," Bwana alimjibu aka- [9]
nena, "Nitapitisha mimi wema wangu wote mbele yako." Huu ndio utukufu wake. Bwana alipita mbele ya Musa, akatamka, "Bwana, Bwana Mungu, mwenye rehema na neema, si mwepesi kwa hasira, na mwingi wa huruma na kweli; awawekeaye elfu huruma, mwenye kusamehe uovu, na kosa, na dhambi." Kutoka 33: 18,19; 34: 6, 7. Naye "mvumilivu, na mwenye wema mwingi," "kwa sababu apendezwa na huruma huyu." Yona 4: 2; Mika 7:18.

Mungu amejifungia mioyo yetu kwake kwa namna nyingi zinazotuonyesha upendo wake; katika viumbe vya ulimwengu, na kwa upendano ulio wema wa wanadamu, Mungu amejaribu kutuonyesha wema wake. Lakini hayo yote hayawezi kutudhihirishia barabara upendo wake jinsi ulivyo, kwa kuwa adui, yaani Shetani, amepofusha macho va kiroho ya wanadamu ili wawe na hofu kwa Mungu; nao humwona Mungu kama ni mkali asiye na huruma. Shetani aliwapoteza wanadamu ili wamdhanie Mungu kuwa ni mkali kabisa—kama mwamuzi aliye na roho ngumu asiyeweza kumwachia mtu. Aliwatilia wanadamu fikara kama Muumba wetu huwachunguachunguа watu ili apate kujua makosa yao na kuwalipiza kisasi. Bwana Yesu alikuja hapa duniani na kuishi kati ya wanadamu kwa kusudi
kuziondolea mbali fikara mbaya hizo, na kutuonyesha upendo wa [10]
Mungn jinsi ulivyo.

Mwana wa Mungu alitoka mbinguni ili awaonyeshe wanadamu Baba aliye mbinguni. "Hakuna mtu aliyemwona Mungu wakati wo wote; Mwana wa pekee aliye katika kifua cha Baba, huyu ndiye aliyefasiri habari yake." "Wala hakuna mtu amjuaye Baba ila Mwana, na ye yote ambaye Mwana apenda kumfunulia." Yoh. 1:18; Mattayo 11:27. Mmoja wa wanafunzi wake alipomwambia, "Tuonyeshe Baba," Yesu alimjibu, "Nimekuwa pamoja nanyi siku hizi zote wala

hukunijua, Filipo? Aliyeniona mimi, amemwona Baba; wasemaje wewe, Tuonyeshe Baba?" Yoh. 14:8, 9.

Yesu alipoeleza namna ya kazi yake aliyojilia kuifanva hapa duniani, alisema hivi,—

> "Roho ya Bwana ni juu yangu,
> Kwa sababu amenitia mafuta kuwahubiri
> maskini habari njema.
>
> Amenituma kuwaponya waliopondeka moyo,
> Kuwatangazia wafungwa kufunguliwa,
> na vipofu kupata kuona tena,
> Kuwaacha huru waliosetwa."
>
> Luka 4:18.

Hiyo ndiyo kazi yake. "Naye akatembea huko na huko, akitenda
kazi njema na kuponya wote walioonewa na Shetani." Matendo
10:38. Katika matendo yake yote alionyesha upendo, rehema na
[11] huruma. Alikuwa katika hali ya kibinadamu ili apate kujua mahitaji
ya wanadamu. Hakuna hata maskini kabisa aliyeogopa kumfikilia
karibu. Watoto pia wakavutwa kwake.

Yesu hakuficha neno lo lote la kweli, lakini aliyesema yote katika moyo wa upendo. Alitumia busara sana na uangalifu na huruma katika maongezi yake na watu. Hakuwafanyia watu jeuri kamwe, hakusema maneno yo yote makali yasipohusu, hakuwahuzunisha watu bila maana. Hakuulaumu udhaifu wa kibi¬nadamu. Alisema kweli tupu, lakini alisema yote katika moyo wa upendo. Alichukizwa sana na hali ya unafiki, na kutokuamini, na uovu; lakini kila aliposema maneno ya lawama na mashtaka, aliyesema kwa masikitiko makubwa. Aliulilia Yerusalemi, mji alioupenda, ambao ulikataa kumpokea yeye aliye Njia, Kweli, na Uzima. Walimkana yeye aliye Mwokozi, lakini hata hivyo akazidi kuwahurumia. Maisha yake yalikuwa ya kujinyima mwenyewe na kuwafikiria wengine. Kila mtu alikuwa na thamani kubwa machoni pake. Ingawa alikuwa Mwana wa Mungu, hakumdharau mwanadamu ye yote; bali aliwaona wote kuwa ni wenye dhambi ambao alikuja kuwaokoa.

Hizo ndizo tabia zake Kristo kama zilivyofunuliwa katika maisha yake. Tena hizo ndizo tabia za Mungu mwenyewe pia. Yesu,

Mwokozi aliye mwema, mwenye huruma, ndiye Mungu hasa aliyed- [12]
hihirishwa katika mwili wa kibinadamu. 1 Tim. 3:16.

Yesu aliishi, akateswa, akafa ili atukomboe. Alikuwa "mtu wa huzuni," ili tuwe washiriki pamoja naye katika furaha ya milele. Naye Mwana Mpendwa wa Mungu, aliyejaa neema na kweli, Mungu alimwacha atoke mahali pa utukufu na kufika hapa duniani, palipoharibika kwa ajili ya dhambi, penye giza ya mauti na laana. Alimkubalia atoke mahali anapopendwa na Babaye na kusifiwa na malaika, aje kuaibika, kudhiliwa, kuchukiwa, na kuuawa. "Adhabu ya amani yetu juu yake." Isa. 53: 5. Mwangalie jinsi alivyo jangwani, katika bustani ya Gethsemane, tena juu ya msalaba. Mwana Mtakatifu wa Mungu akachukua mwenyewe uzito wa dhambi ya wanadamu. Yeye aliyekuwa na umoja na Mungu, akaona mwenyewe moyoni mwake ubaya wa hali ya kutengana na Mungu, ndiyo hali ya wanadamu kwa ajili ya dhambi. Kwa ajili ya matengano hayo akaona uchungu moyoni naye akalia, "Mungu wangu, Mungu wangu, mbona umeniacha?" Mattayo 27:46. Uzito wa dhambi, jinsi ulivyo mbaya kupita kiasi, na jinsi unavyoleta kutengana na Mungu—huu ndio uliouvunja moyo wa Mwana wa Mungu.

Lakini Yesu hakujitoa kuwa dhabihu kubwa hivi makusudi
kumtilia Baba yake moyo wa kuwapenda wanadamu na kuwaokoa. [13]
Sivyo! "Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akampeleka Mwana wake wa pekee, ili mtu aliye yote amwaminiye asipotee, bali apate uzima wa milele." Yoh. 3:16. Tangu zamani Baba yetu aliye mbinguni ametupenda, si kwa ajili ya upatanisho alioufanya Yesu, ila kwa kuwa Mungu mwenyewe alitupenda, naye akamkubali Yesu afanye upatanisho huo. Kristo ndiye njia ambayo kwayo Mungu hutuonyesha upendo wake kwetu. "Yaani, Mungu alikuwa ndani ya Kristo, akiupatanisha ulimwengu na nafsi yake." 2 Wakor. 5:19. Mungu alipata maumivu pamoja na Mwanawe. Huko Gethsemane, na kwa kufa kwake Kalwari, Mungu alijitoa kwa ajili ya wokovu wetu.

Yesu alisema, "Ndio maana Baba anipenda, kwa sababu nauweka uzima wangu ili niutwae tena.' Yoh. 10:17. Yaani, ni kama Yesu angesema hivi: "Baba yangu amewapendeni sana hata anazidi kunipenda mimi kwa sababu ya kujitoa maisha yangu kwa ajili yenu. Mimi nikawa ninajitoa badala yenu tena kuwa kama dhamana yenu, na kwa jinsi nilivyochukua makosa yenu na adhabu ambayo ili-

wapasa ninyi, kwa hayo Baba yangu huzidi kunipenda mimi; kwa sababu ya Dhabihu yangu, Mungu aweza kuwa mwenye haki tena kumhesabia haki yule amsadikiye Yesu."

[14] Hakuna awezaye kutuokoa, ila Mwana wa Mungu tu; kwa kuwa yeye pekee aliyekuwa pamoja na Baba, ndiye awezaye kumsifu na kueleza tabia zake. Yeye tu aliyeujua upendo wa Mungu ndiye awezaye kuudhihirisha upendo ule barabara. Hakuna njia nyingine ya kutuonyesha jinsi Mungu anavyowapenda wanadamu waliopotea, ila kwa njia hii moja tu, yaani ya Kristo alivyojitoa na kufa badala yao.

"Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akampeleka Mwana wake wa pekee." Yoh. 3:16. Mungu alimtoa Mwanawe aishi kati ya wanadamu ili azichukue dhambi zao, apate kuadhibiwa badala yao, na kuwatolea maisha yake kama dhabihu; pia Mungu akamtoa awe katika hali moja na wanadamu ambao wamepotea, na kushirikiana nao katika mambo ya maisha yao na haja zao zote. Yeye aliyekuwa mamoja na Mungu amejiunga na wanadamu kwa namna isiyoweza kuvunjwa. Yesu "haoni haya kuwaita ndugu zake." (Waeb. 2:11); yeye ndiye Dhabihu yetu, Mwombezi wetu mbele ya Mungu, Ndugu yetu aliye katika mfano wa kibinadamu na kushirikiana nao hao ambao amekuja kuwaokoa—Yeye ndiye Mwana wa mwanadamu. Alifanya hayo yote ili awakomboe wanadamu katika dhambi na hali yake mbaya, naye mwanadamu
[15] apate kujua upendo wake Mungu na kushirikiana naye katika hali ya furaha na usafi.

Tukifahamu kimo cha wokovu wetu, jinsi Mwana wa Mungu alivyokufa kwa ajili yetu, imetulazimu kutambua jinsi tunavyoweza kuwa watu walio bora katika Kristo. Mtume Yohana alipofahamu upendo wa Mungu jinsi ulivyo mkubwa mno, aliona hana budi kumcha Mungu na kumsujudu moyoni mwake. Upendo huo, jinsi ulivyo wa huruma na rehema, ni upendo mkubwa usioweza kusemeka; naye Yohana alisema, "Fahamuni, ni pendo la namna gani alilotupa Bwana, kuitwa wana wa Mungu." 1 Yoh. 3:1. Mungu amewaona wanadamu kuwa ni wenye thamani kubwa ya namna gani! Kwa kuanguka katika kufanya dhambi, wanadamu wakawa chini ya mamlaka ya Shetani. Lakini kwa kumwamini Kristo na kutolewa kwake, waweza kuwa wana wa Mungu. Kristo alikuwa katika hali ya kibinadamu ili apate kuwasaidia wanadamu. Nao

wenye dhambi wakiwa wanashirikiana naye Kristo, watageuzwa hali yao, na kustahili kuitwa "wana wa Mungu."

Upendo wa ajabu huo, hauwezi kulinganishwa na kitu cho chote! Wana wa Mfalme aliye mbinguni! Ahadi ya kupendwa sana! Jambo la maana sana lifaalo kufikiriwa! Upendo usio na kifani, jinsi Mungu
alivyoupenda ulimwengu usiompenda! Fikara hiyo huutiisha moyo [16]
na kuutuliza ili ufungwe kwake Mungu na kufanya mapenzi yake. Na jinsi tunavyozidi kuzichungua tabia za Mungu, na kufahamu jinsi alivyotufanyia kwa kufa kwake Kristo msalabani, ndivyo tunavyozidi kuona kama Mungu ndiye mwenye rehema na huruma, na ndiye awezaye kuwasamehe wenye makosa, naye ni mwenye haki, naye huwapenda wanadamu kwa upendo mkubwa upitao kiasi cha upendo wa mama kwa watoto wake.

Mapenzi ya milele
    Ndiyo yanipendayo;
Yalinipenda mbele,
    Sina fahamu nayo;
Sasa amani yake
    Tele rohoni mwangu,
Ni mimi kuwa wake,
    Na Yeye kuwa wangu.
Ni mimi kuwa wake,
    Na Yeye kuwa wangu.

    Wake hata milele,
Si kutengana tena;
    Hunipa raha tele
Moyoni mwangu, Bwana
    Hiyo nchi na mbingu
Zitatoweka zile;
    Ni wake, Yeye mbwangu,
Milele na milele,
    Ni wake, Yeye mbwangu,
Milele na milele.

[17] # Sura 2—Jinsi Mwenye Dhambi Anavyomhitaji Kristo

HAPO mwanzo binadamu alipewa uwezo bora na fikara safi. Alikuwa mkamilifu katika mwili wake, naye akawa katika hali ya umoja na Mungu. Fikara zake zilikuwa safi na makusudi yake yakawa matakatifu. Lakini kwa ajili ya kutomtii Mungu, uwezo wake uligeuka ukawa mbaya, tena badala ya upendo akawa akijifikiria nafsi yake mwenyewe. Dhamiri yake ikapungua nguvu kwa sababu ya kufanya dhambi, hata yeye mwenyewe kwa nguvu zake peke yake alikuwa hawezi kushindana na maovu. Alikuwa chini ya mamlaka ya Shetani, naye mwanadamu angalikuwa katika hali hiyo milele kama Mungu asingaliondoka na kumsaidia. Ilikuwa nia ya mshawishi, yaani Shetani, kuyapinga maazimio mema ya Mungu katika kumwumba binadamu, na kujaza dunia ubaya na ukiwa. Na hatimaye angesema kwamba mabaya hayo yote yalitokea kwa ajili ya kazi ya Mungu katika kumwumba binadamu.

[18] Katika hali yake ya kutokuwa na dhambi mwanzoni, mwanadamu akawa na furaha katika kuzungumza na Yule "ambaye ndani yake zimo hazina zote za hekima na maarifa." Wakol. 2:3. Lakini baada ya kufanya dhambi mwanadamu hakuweza kufurahishwa na hali ya utakatifu, naye alitaka kujificha mbali na macho ya Mungu. Hata sasa hiyo ndiyo hali ya moyo usioongoka. Haupatani na Mungu, tena hauna furaha katika maongezi naye. Mwenye dhambi asingeweza kuwa na furaha mbele ya Mungu; angewaepuka watakatifu. Kama angeweza kuruhusiwa kuingia mbinguni, asingekuwa na furaha huko. Naye asingeweza kushirikiana nao walio mbinguni katika hali ya kuwa na roho inayopatana na Mungu, yaani roho isiyofikiria nafsi yake yenyewe, bali huwa ya kuwafikiri wengine kwa upendo. Fikara zake, mambo anayoyapenda, na maazimio yake yote, vyote hivi vingemfanya mwenye dhambi kuwa mgeni kabisa kati ya wateule wa Mungu; angekuwa hawezi kulingana nao. Angeona mbinguni kama ni mahali pabaya kwake; angetaka kujificha mbali na uso wake yeye aliye nuru na

furaha ya watakatifu wa Mungu. Wabaya hawatazuiliwa kuingia mbinguni kwa sababu ya amri kali ya Mungu isiyo na maana, bali watazuiliwa kwa kuwa wenyewe hawana tabia inayopatana na hali ya mbinguni. Utukufu wa Mungu ungekuwa kama moto wa kuwa-teketeza, nao wangetaka kufichwa wasimwone uso wake yeye aliyek- [19]
ufa kuwakomboa watu. Ufunuo 6:15-17.

Sisi wenyewe kwa nguvu zetu hatuwezi kujiokoa katika shimo la uovu ambamo tumeangukia. Mioyo yetu mibaya kabisa, nasi hatuwezi kuigeuza. "Awezaye nani kutoa kilicho safi katika kisicho safi? si hata mmoja." "Kwa kuwa ile nia ya mwili ni uadui juu ya Mungu, kwa maana haitii sheria za Mungu wala haiwezi." Ayub 14:4; Warumi 8:7. Elimu, ustaarabu, kujitawala nia, kujibidisha, hivi vyote vinafaa, lakini katika kazi hii ya kuugeuza moyo haviwezi kitu kamwe. Pengine vyaweza kumfanya mtu awe na mwenendo mzuri mbele ya watu; lakini haviwezi kuigeuza asili yake na moyo wake. Nguvu isiyokuwa yake mwenyewe lazima itumike moyoni mwake ili apate uzima mpya utokao juu, hapo ndipo binadamu atakapoweza kugeuza hali yake ya kufanya dhambi na kuwa katika hali ya usafi. Nguvu hiyo ndiyo Kristo. Ni yeye tu ambaye anaweza kuwavuta watu kwa Mungu ili wawe safi. Mwokozi alisema, "Mtu asipozaliwa mara ya pili," yaani kuzawa na Roho, "hawezi kuuona ufalme wa Mungu." Yoh. 3:3. Maana yake, isipokuwa amepata moyo mpya, nia mpya, maazimio mapya, na kuishi katika uzima mpya, "hawezi kuuingia ufalme wa Mungu." Yoh. 3:5. Tusifikiri [20]
kwamba inatosha kuziongeza zile tabia njema ambazo amezipata mtu tangu asili. "Mwanadamu wa tabia ya asili hayapokei mambo ya Mungu; maana kwake ni mapumbavu, wala hawezi kuyajua, kwa kuwa yanatambulikana kwa jinsi ya rohoni." Usistaajabu kwa kuwa nilikuambia, Hamna budi kuzaliwa mara ya pili." 1 Wakor. 2:14; Yoh. 8:7. Imeandikwa juu ya Kristo, "Ndaniyake ndimo ulimokuwa uzima, nao uzima ulikuwa nuru ya watu," tena "hapana jina jingine chini ya mbingu walilopewa wanadamu litupasalo kuokolewa nalo." Yah. 1:4; Matendo 4:12.

Haitoshi kujua namna ya upendo, na neema ya Mungu. Haitoshi kutambua tu namna ya amri zake, jinsi zilivyo za haki. Mtume Paulo aliyajua haya yote, akasema, "Nakiri ya kuwa sheria ile ni njema." "Torati ni takatifu, na ile amri takatifu na ya haki na wema." Warumi 7:16,12. Naye akazidi kusema kwa uchungu wa moyo,

"Mimi ni mtu wa mwilini, nimeuzwa chini ya dhambi." Warumi 17:14. Alitamani sana kuwa na usafi na uadilifu kamili, ambavyo yeye mwenyewe kwa nguvu zake hakuweza kuvipata, naye akalia, "Ole wangu mimi binadamu! nani atakayeniokoa na mwili huu wenye kunifisha." Warumi 7:24. Kila anayelia hivyo hujibiwa neno moja tu. "Tazama, Mwana-Kondoo wa Mungu, aichukuaye dhambi ya ulimwengu!" Yoh. 1:29.

[21] Kwa njia nyingi na mifano mingi Roho Mtakatifu amejaribu kuwafundisha watu mambo hayo, na kuwaeleza dhahiri wale watakao kuokolewa katika dhambi. Yakobo alipokimbia baada ya kumdanganya Esau, aliona moyoni mwake kuwa ana hatia; naye akaogopa akifikiri labda makosa yake yamemtenga mbali na Mungu, naye akawa na huzuni moyoni mwake. Alipolala usingizi usiku ule, akaota ndoto; aliona ngazi iliyotoka chini mpaka mbinguni; tena malaika wa Mungu wakawa wakipanda na kushuka; tena kutoka mahali patakatifu juu akasikia sauti ya Mungu ikimwambia maneno ya kumtia moyo. Mambo hayo yakamjulisha Yakobo kwamba yuko Mwokozi, tena aliona jinsi alivyoweza kurudishwa tena kupatana na Mungu. Ile ngazi ya ndoto ilikuwa mfano wa Yesu, ambaye ni njia ya pekee kwa wanadamu kuweza kumfikia Mungu.

Huu ndio mfano Yesu alioutaja alipozungumza na Nathanael, akisema, "Mtaziona mbingu zimefunguka, na malaika wa Mungu wakipanda, wakishuka juu ya Mwana wa Adamu. Yoh. 1:51. Katika maasi yake, binadamu alijitenga mbali na Mungu; wanadamu walikuwa hawawezi kuzungumza nao wa mbinguni kama walivyokuwa wamezoea kufanya zamani. Lakini kwa ajili ya Kristo tumepata
[22] njia ya upatanisho. Malaika waweza kuja kusema na wanadamu na kuwasaidia. Tena hata kama binadamu wamekuwa wabaya kwa ajili ya dhambi, katika Kristo waweza kupata nguvu ya kushindana na maovu. "Kila kutoa kwema, na kila kitolewacho kilicho kamili, chatoka juu," kwa Mungu. Yakobo 1:17.

Binadamu hawawezi kuwa na sifa njema ya kweli bila Mungu. Tena Kristo ndiye njia ya pekee kwa kumfikia Mungu. Asema, "Ndimi niliye njia, na kweli, na uzima; mtu haji kwa Baba bila kwa mimi." Yoh. 14:6. Moyo wa Mungu huwafikiria watoto wake duniani kwa upendo mkubwa mno. Alipomtoa Mwanawe wa pekee kwa ajili yetu, alikuwa kama anatoa kwetu ubora wote wa mbinguni. Maisha ya Mwokozi hapa duniani, kufa kwake, na maombezi yake

huko mbinguni, msaada wa malaika, maombezi ya Roho Mtakatifu mioyoni mwetu—hivyo vyote hutuonyesha jinsi Baba yetu aliye mbinguni awapendavyo wanadamu, tena hutumia njia nyingi ili awakomboe.

Heri tufikiri sana habari za Mwokozi wetu, jinsi alivyojitoa kama dhabihu kwa ajili yetu! Ajabu sana, mambo haya! Imetupasa kufahamu kwamba katika Kristo tumepewa thawabu kubwa kupita kiasi, ili apate kutuokoa na kuturudisha kwa Mungu. Tufikiri tena yote ambayo Mungu amewaahidia waaminifu wake! Ameahidi thawabu kubwa kwao wanaofanya haki: kufurahishwa mbinguni, kukaa na malaika na kuwa na umoja nao, kuongea uso kwa uso na [23]
Mungu na Mwanawe, na kujua upendo wao hasa jinsi ulivyo, tena kuzidi kuelimishwa milele. Je, hivyo vyote havitoshi kutuonyesha kuwa ni lazima tumtolee Mwokozi wetu mioyo yetu kwa upendo wetu, ili tuwe watumishi wake milele?

Bali, hukumu ya Mungu imetangazwa jinsi itakavyokuwa juu ya dhambi na wenye dhambi, kupata adhabu isiyoepukika, kuwa katika hali ya udhilifu, na uharibifu wa mwisho; hivyo vyote vimetangazwa katika Neno la Mungu kutuonya tusiwe watumishi wa Shetani.

Laiti tungefikiri sana rehema ya Mungu! Angeweza kufanya nini tena zaidi ya hivyo vyote? Heri tulingane naye ambave ametupenda sana kwa upendo wa ajabu. Heri tufuate njia yake, tena tutumie nguvu zake ili tupate kugeuka kuwa katika mfano wake, tuingie tena katika hali ya kushirikiana na malaika kama walivyokuwa wanadamu mwanzoni, hali ya umoja na Baba aliye mbinguni na Mwanawe pamoja.

[24]

# Sura 3—Kutubu

BINADAMU awezaje kuhesabiwa kuwa ana haki mbele ya Mungu? Mwenye dhambi awezaje kusahihishwa na kuwa kama asiye na makosa machoni pake? Kristo ndiye njia tu ya kutupatanisha na Mungu na kutuweka katika hali ya usafi. Lakini twawezaje kufika kwake Kristo? Watu wengi wangali wakisema kama walivyosema wengine siku ile ya Pentekote: "Tufanyeje?" Jibu la Petro lilikuwa hivi: "Tubuni." Pengine pia alisema hivi, "Tubuni basi, mrejee, ili dhambi zenu zifutwe." Matendo 2:38; 3:19.

Kutubu maana yake ni hivi: kuhuzunika kwa ajili ya dhambi. tena kujitenga mbali nayo. Hatuwezi kuacha kufanya makosa mpaka tumetambua ubaya wake: tena hali yetu katika maisha yetu haitabadilika kamwe mpaka tumeitenga dhambi mbali na mioyo yetu.

Kuna watu wengine ambao hawafahamu asili ya kutubu jinsi ilivyo halisi. Wengi huhuzunika kwa ajili ya makosa yao, tena hujaribu kuongoka katika mwenendo wao mbele ya watu, kwa kuwa wanaogopa adhabu ambayo watajipatia kwa ajili ya matendo
[25] mabaya. Lakini huku si kutubu kama Mungu anavyotaka. Wao hufikiria adhabu zaidi ya ubaya wa makosa yao. Hivyo ndivyo alivyofanya Esau alipoona ya kwamba amepotewa kabisa na urithi wake. Balaam pia, alipotiwa hofu sana kwa ajili ya kumwona malaika aliyesimama mbele yake na upanga mkononi, akakubali kutiwa hatiani asije akauawa; walakini hakutubu kwa kweli, hakugeuka moyo, hakuchukizwa na maovu. Yudas Iskarioti, alipomsaliti Bwana, alisema, "Nalikosa nilipoisaliti damu isiyo na hatia." Mattayo 27:4.

Alishurutishwa kukiri makosa yake alipoona moyoni mwake jinsi alivyostahili kuhukumiwa na Mungu kwa kosa lake. Lakini kitu kilichomtia hofu kilikuwa hukumu na adhabu ya Mungu; hakuhuzunika sana moyoni na kuingiwa na majuto kwa kuwa amemsaliti yule mtakatifu Mwana wa Mungu, au kwa kuwa amemkana Mtakatifu wa Israeli. Farao pia; alipoona maumivu ya Mungu alikiri makosa yake ili apate kuepuka adhabu; lakini mapigo yalipokoma, alizidi

kufanya kiburi. Watu hao wote walililia mambo yaliyotokea kwao kwa ajili ya makosa yao, lakini hawakuwa wakihuzunika na kujuta kwa ajili ya makosa yenyewe na ubaya wake.

Lakini kama mwenye dhambi anajitoa kuwa chini ya utawala wa Roho Mtakatifu, ndipo dhamiri yake itakaposafishwa, ataona barabara jinsi alivyo katika hali ya kufanya dhambi, atafahamu [26]
maana ya usafi wa amri za Mungu ambazo ndizo msingi wa utawala wake. "Kulikuwako nuru halisi, imtiayo nuru kila mtu ajaye katika ulimwengu." Yoh. 1:9. Nuru ile, ndiye Kristo, humtia mtu nuru moyoni, mambo ya siri hufunuliwa, na yule mwenye dhambi hujiona jinsi alivyo na hatia machoni pa Mungu mwenye haki kabisa. Pia huelewa na upendo wa Mungu na uzuri wa kuwa katika hali ya usafi na utakatifu; hutamani kusafishwa na kupatana nao walio mbinguni.

Sala ya Daudi baada ya kuanguka kwake dhambini hutudhihirishia vizuri namna ya kweli ya kuhuzunika na kujutia maovu. Hakutaka kulipunguza kosa lake, wala kuepuka hukumu ilivyokuwa stahili yake. Daudi aliona kosa lake jinsi lilivyokuwa kubwa mno; aliona unajisi wa moyo wake; akachukizwa sana na kosa lake. Hakuomba ili apate kuachiliwa tu, akaornba pia apate kusafishwa moyoni mwake. Akatamani kuingia katika hali ya usafi na kuwa mmoja na Mungu. Akaomba hivi:—

Heri aliyesamehewa makosa, aliyestirikiwa
dhambi,
Heri mwanadamu, Bwana asiyemhesabia hatia,
Rohoni mwake isipokuwa hila."

Zaburi 32:1, 2.

Unirehemu, Ee Mungu, kwa jinsi ulivyo mwema:
Rehema zako zilivyo kuu, ufute makosa yangu.
Unioshee kabisa hatia yangu, unitakasie dhambi [27]
zangu.
Kwani nayajua makosa yangu: na dhambi yangu
mbele yangu daima . . . .
Unisafishe kwa ezobu, nami nitakuwa safi;
Unioshe, nami nitakuwa mweupe kuliko theluji. . . .
Uniumbie moyo safi, Ee Mungu,

Ufanye ndani yangu roho aminifu.
Usinitupe usoni pako;
Usiniondolee roho yako takatifu.
Unirudishie furaha ya wokovu wako:
Unichukue kwa roho bora . . . .
Uniponye kwa damu, Ee Mungu, Mungu wa wokovu wngu;
Na ulimi wangu utaiimba haki yako.”

Zaburi 15:1-14.

Kutubu kwa namna ile hakuwezekani kwetu sisi kwa uwezo wetu wenyewe; kunawezekana katika Kristo tu. Hapo ndipo wengi hupotea katika kudhani kwamba hawawezi kuja kwake Kristo isipokuwa kwanza wamekwisha kutubia dhambi zao. Ni kweli mtu lazima kutubia dhambi zake kwanza, ndipo Mungu atamwachilia; kwani bila masikitiko moyoni kwa ajili ya makosa, mwenye dhambi hawezi kufahamu jinsi anavyomhitaji Mwokozi. Je, mwenye dhambi hana budi kungoja kumfikia Kristo mpaka ametubu?

Katika Biblia, Neno la Mungu, hatusomi kwamba mwenye dhambi hana budi kutubu kabla ya kukubali mwito wa Kristo aliye-
[28] sema, ” Njooni kwangu, ninyi nyote msumbukao na wenye mizigo, nami nitawapumzisha.” Mattayo 11: 28. Ni uwezo wa Kristo unaowezesha watu kutubu kwa kweli. Petro ameeleza mambo haya dhahiri aliposema, “Mtu huyo Mungu amemtukuza kwa mkono wake wa kuume, awe Mkuu na Mwokozi, awape Waisraeli toba na masamaha ya dhambi.” Matendo 5:31. Kwa kadiri tusivyoweza kusamehewa dhambi bila Kristo, ndivyo tusivyoweza kutubu pasipo nguvu za Roho ya Kristo mioyoni mwetu. Kristo ndiye asili ya kila fikara njema. Yeye tu ndiye awezaye kuutia moyo fikara ya kushindana na maovu. Kila aonaye moyoni mwake haja ya kuwa na kweli na usafi, kila asadikiye hali yake ya dhambi, huwa anashuhudia kwamba Roho Mtakatifu yumo moyoni mwake.

Yesu amesema, “Nami nikiinuliwa juu ya nchi nitavuta wote kwangu.” Yohana 12:32. Mwenye dhambi hana budi kumwona Yesu kama Mwokozi wetu aliyekufa kwa ajili ya dhambi za ulimwengu; nasi tukimwona msalabani kwa macho ya kiroho, tutazidi kufahamu mambo ya wokovu, tena wema wa Mungu utatuongoza ili tutubu. Hatuwezi kufahamu barabara upendo wa Kristo jinsi ulivyomshu-

rutisha afe kwa ajili yetu; lakini upendo huo huivuta mioyo yetu kwake.

Pengine watu huona aibu kwa ajili ya matendo yao mabaya, nao huacha kufanya maba- ya mengine, kabla hawajajua kwamba Kristo [29] Yesu ndiye anayewavuta kwake. Naye akizidi kuwavuta macho ili wamwangalie msalabani na jinsi alivyopata maumivu kwa dhambi zao, wao nao huzidi kufahamu ubaya wa mwenendo wao wenyewe, na kujua namna ya haki yake Kristo. Nao huwa wanaanza kusema, "Je, dhambi ni kitu gani, ikiwa imetakiwa dhabihu kubwa namna hii kwa kumwokoa mwenye dhambi? Je, upendo wa namna hii, maumivu haya yote, udhilifu huu, hivi vyote vilikuwa ni lazima ili sisi tusipotee mbali, bali tupewe uzima wa milele?"

Isipokuwa mtu amekataa kuvutwa kwake Kristo, Roho yake itazidi kuugeuza moyo wake mpaka ametubu na kuongoka moyo. Mambo ya kidunia hayawezi kutuliza moyo wa binadamu. Furaha ya kweli hupatikana katika kumjua Kristo tu. Kwa njia nyingi, zinazojulikana na zisizojulikana, Mwokozi anawavuta watu kwake ili waitoe mioyo yao mbali na anasa ya kidunia na kujua mibaraka ya Mungu isiyo na mwisho. Wewe ambaye umetamani moyoni mwako kupata kilicho bora zaidi ya vyote vya kidunia, heri ujue kwamba kutamani huko ni ile sauti ya Mungu anayosema kwako.

Pengine tumejisifu kwamba maisha yetu yamekuwa safi, dhamiri yetu imekuwa barabara, hatuna haja ya kujitweza moyo mbele ya Mungu kama wabaya wengine; lakini nuru ya Kristo ikituangaza [30] roho zetu, tutaona hali yetu halisi, jinsi tunavyokuwa na unjisi machoni pake; ndipo tutakapofahamu jinsi haki yetu inavyokuwa kama vitambaa vichafu, tena ni damu yake Kristo peke yake ambayo huweza kutusafisha mioyo unajisi wa dhambi, na kute ngeneza mioyo yetu tena kuwa katika hali ya kufanana naye.

Mwonzi mmoja wa nuru ya utukufu wa Mungu ukiupenya moyoni, umetosha kutudhihirishia hali yetu katika dhambi, udhaifu wetu na upungufu wetu. Hivyo twatambua tamaa zetu zisizo safi, jinsi tunavyomkana Mungu mioyoni mwetu, na jinsi midomo yetu inavyotoa maneno yasiyofaa. Roho ya Mungu ikiupenya moyo ndani, na kumjulisha mtu hali yake ya kumwasi Mungu, hapo ndipo hujichukia sana akijilinganisha na Kristo jinsi alivyo safi bila mawaa yo yote.

Nabii Daniel alipouona utukufu wa Mungu aliyetumwa kwake, akabaini moyoni mwake, jinsi udhaifu na ukosefu wake ulivyokuwa mkubwa. Akasema, "Hazikusalia nguvu ndani yangu: kwani uzuri wangu umebadilika mwangu kuwa uharibifu, wala sikuwa na nguvu.' Danieli 10:8. Mtu akijiona hivyo kuwa si safi, ndivyo atakavyotaka kuwa na moyo safi na kuingia katika hali ya kupatana na amri za Mungu na kufanana naye Kristo.

[31] Paulo alipojichunguza aliona kwamba ka- tika matendo ya nje, alikuwa, hana makosa; (Wafil. 3:6); lakini alipotambua matakwa ya sheria kwa njia ya kiroho, alijiona kuwa ni mwenye dhambi kabisa. Alipojipima kwa maneno ya sheria za Mungu jinsi wanavyopima binadamu kwa matendo ya nje, Paulo alijiona kwamba amekuwa katika hali ya kutofanya makosa, hakuwa na hatia; lakini alipoichunguza na kujua maana hasa ya sheria, akajiona jinsi Mungu alivyomwona yeye, kuwa ni mwenye dhambi kabisa, naye akajishusha moyo na kuungama makosa yake. Alisema, "Na mimi nalikuwa hai hapo kwanza bila sheria; ila ilipokuja ile amri, dhambi ilihuika, na mimi nikafa." Warumi 7:9. Alipoona asili ya sheria, jinsi ilivyokuwa ya kiroho, ndipo alipoona dhambi jinsi ilivyokuwa ya uovu, naye hakujiona tena kuwa ni bora.

Mungu hazioni dhambi zote kuwa ni sawa; zinakadirika mbalimbali machoni pa Mungu kama vile zinavyokadirika mbalimbali machoni pa binadamu pia. Lakini tendo baya liwalo lote, ingawa linaonekana kuwa ni dogo machoni pa binadamu, halihesabiwi dogo machoni pa Mungu. Hukumu ya kibinadamu si kamili, kwa kuwa huona sehemu moja tu; hawezi kujua nia ya ndani ya mtu; walakini Mungu hujua moyo tena hukadirisha mambo jinsi yalivyo halisi. Mlevi hudharauliwa na wenziwe na kuambiwa kwamba dhambi
[32] yake itamzuia asiingie mbinguni; lakini mara nyingi makosa kama kufanya kiburi, kujifikiria mwenyewe bila kufikiri wengine, kuwa na choyo, na mengineyo kama hayo hayakadiriwi na binadamu. Lakini makosa kama hayo yanachukiwa sana na Mungu; kwa kuwa yamekuwa kinyume kabisa cha sifa yake Mungu mwenyewe. Yule ambaye hufanya dhambi zinazohesabiwa na binadamu kuwa ni mbaya sana—yaani ulevi, kuiba uzinzi na zingenezo —mtu kama huyo huona aibu na namna anavyomhitaji Kristo; lakini mwenye kufanya kiburi haoni lazima yake, naye humfungia Kristo asiingie moyoni mwake, na kwa hivyo hukosa kupata mibaraka yake.

Yule mtoza ushuru aliyeomba, "Mungu uniwie radhi mimi mwenye dhambi," alijiona kwamba yu mtu mbaya sana, na wengine pia wakamwona hivyo; lakini yeye alijua shida yake, naye alimletea Mungu mzigo wake mzito wa dhambi kwa haya, ili Mungu amrehemu na kumtoa katika utumwa wa dhambi. Luka 18:13. Yule mfarisayo aliyefanya kiburi na kujifanya mwenye haki katika sala yake, akaonyesha kwamba amemfungia Roho Mtakatifu mlango wa roho yake, asiingie. Kwa hivyo hakujiona jinsi alivyo na unajisi; hakuona jinsi anavyouhitaji msada wa Kristo, naye hakupata kubarikiwa kamwe.

Ukitambua hali yako jinsi ulivyo katika dhambi, usingoje [33]
kumwendea Kristo mpaka umejaribu mwenyewe kujitengeneza kuwa safi. Wengi hufikiri kwamba hawawezi kumfikia Kristo kwa kuwa ni wabaya. Je, unafikiri utapata kuwa mwema kwa uwezo wako mwenyewe? "Aweza Mkushi kubadili ngozi yake, au chui madoadoa, ndipo nanyi mtaweza kutenda mema, mliofundishwa kutenda mabaya." Yer. 13:23. Hakuna msaada kwetu ila kwa Mungu tu. Sisi wenyewe hatuwezi kitu. Imetulazimu kwenda kwake Kristo kama tulivyo.

Hata hivyo tusijidanganye katika kufikiri kwamba Mungu, kwa neema yake, atawaokoa hata wale wanaotupilia mbali neema yake na rehema zake. Afikiriye hivyo, afadhali aitazame Kalwari. Kwa kuwa hakuna njia nyingine ya kuwaokoa watu, kwa kuwa bila dhabihu aliyoifanya Kristo katika kufa kwake msalabani, binadamu asingeweza tena kuwa katika hali ya kupatana na watakatiu wa mbinguni —kwa hivyo Kristo alichukua mwenyewe dhambi za wakosaji, akaadhibiwa kwa ajili yao. Upendo wa Mwana wa Mungu, maumivu yake, na kufa kwake, hivi vyote hushuhudia jinsi dhambi inavyokuwa kubwa mno machoni pa Mungu; pia mambo hayo yatudhihirishia kwamba hakuna njia ya kuokoka na kutoka katika utawala wa uovu, hakuna matumaini ya uzima bora wa milele, ila kwa kujiweka chini ya mamlaka yake Kristo na kumtii.

Wenye mioyo migumu wasiotubu, pengine hujisingizia [34]
wakisema hivi juu yao wanaojidai kuwa ni Wakristo, "Hata mimi ni mtu mwema kwa kadiri wanavyokuwa wema wale. Wao hawajinyimi zaidi yamimi; mimi najiweza jinsi wafanyavyo. Wao pia hupendezewa na anasa ya kidunia kama nipendezewavyo mimi." Hivyo watu kama hao hujisingizia kwa ajili ya makosa ya wengine

ili wasifanye wajibu wao. Lakini kujisingizia hivyo haifai kitu; kwa kuwa Bwana ametuwekea mfano usio wa kibinadamu: Mwana wa Mungu, asiye na hila wala kosa lo lote, yeye ndiye mfano wetu. Wale ambao hunung'unika kwa ajili ya mwenendo mbaya wa wengine wanaojidai kuwa ni Wakristo, imewapasa kufuatisha maisha na matendo ya Kristo, na kuwatolea wengine namna ya mfano ulio bora. Wamejua namna iwapasavyo Wakristo kufanya; hivyo wakikosa wenyewe kufanya yaliyo mema, makosa yao ni makubwa zaidi.

Tuangalie tusifanye usiri. Tusichelewe kuziacha dhambi zetu na kutaka usafi wa moyo katika Yesu. Watu wengi hukosa katika jambo hilo; hukawia katika kujitoa kuwa wa Kristo; wafanyao hivyo wanaehagua kuishi katika hali ya kufanya dhambi. Kitu ambacho tunakosa kukishinda, kitatushinda sisi na kutuangamiza.

[35] Adamu na Hawa walijidanganya kwamba kula matunda yaliyokatazwa si kosa kubwa linaloweza kuadhibiwa kama Mungu alivyosema. Lakini katika jambo hilo dogo walihalifu amri takatifu ya Mungu, amri isiyobadilika; kwa hivyo binadamu akatengwa mbali na Mungu, tena kifo na taabu viliingia duniani mwetu. Kufa kwake Yesu katika Kalwari, kama dhabihu, kulikuwa njia ya pekee ya kufanya upatanisho tena kati ya Mungu na binadamu. Tusidhanie dhambi kwamba ni kitu kisicho na maana sana.

Kila tendo baya, kila mara unapoidharau na kuitupilia mbali neema ya Kristo, moyo wako huzidi kuwa mgumu, nia yako huzidi kuwa mbaya, nawe huzidi kuwa katika hali ya kutosikia maombezi ya Roho Mtakatifu moyoni mwako.

Watu wengi huwa wakijituliza dhamiri na mawazo yanayowasumbua, wakidhani kwamba wataweza kugeuza mwenendo wao mbaya wakati wo wote watakapo; wao hufikiri kwamba waweza kuacha na kutosikia wito wa Roho wakati mwingine, wakitumaini watachomwa moyoni mara kwa mara baadaye. Lakini sivyo. Hata tabia mbaya moja tu, ama namna moja ya tamaa isiyofaa, ikidumu moyoni itathibitisha moyo katika kutompenda Mungu. Kwa maonyo yote katika Biblia juu ya kuchezacheza na maovu, lile la kututisha
[36] zaidi ndilo hili, linalosema, "Maovu yake yatamkamata mwovu mwenyewe, naye atashikwa kwa kamba ya dhambi yake." Methali 5: 22.

Kristo amekuwa tayari kutuweka huru kwa dhambi, lakini halazimishi watu kwa nguvu; kama mtu amekusudia kufanya dhambi,

naye *hataki* kupata uhuru katika Kristo, *asitake* kupokea neema yake, Kristo angefanya nini tena? Mtu akifanya hivyo amejiharibu mwenyewe kwa ajili ya kukana upendo wake Kristo. Tumeambiwa, "Sasa ndio wakati uliokubalika sana; tazama, sasa ndio siku ya wokovu." "Leo, kama mtasikia sauti yake, msifanye migumu mioyo yenu." 2 Wakor. 6:2; Waeb. 3:7,8.

"Wanadamu hulitazama umbo la nje, lakini Bwana hutazama moyo." 1 Sam. 16:7. Mungu huutazama moyo wa kibinadamu jinsi ulivyo mkaidi, panapokuwa unajisi na udanganyifu. Mungu hutujua kabisa, moyo wetu, dhamiri yetu, makusudi yetu na maazimio yetu. Nenda kwake jinsi ulivyo na moyo usio safi, ukamwambie, "Unitafutetafute, Ee Mungu, unijue moyo; unijaribu, unijue mawazo; utazame kama njia ya kukasirisha mwangu, unichukue kwa njia ya milele." Zaburi 139:23, 24.

Watu wengi hukubali dini katika akili zao tu, na kufanya matendo matupu ya nje tu, bila kugeuzwa moyo. Imekupasa kuomba hivi, "Uniumbie moyo safi, Ee, Mungu; ufa- nye ndani yangu roho [37]
aminifu." Zaburi 51:10. Ni heri ujitahidi ili usipotewe na uzima wa milele, kwa jinsi watu wafanyavyo kujiokoa maisha ya sasa wakiwa hatarini. Ni heri ufanye bidii katika kusoma Neno la Mungu pamoja na kuomba. Katika Neno hilo, kwa njia ya amri za Mungu na maisha ya Kristo, tumeonyeshwa asili ya utukufu, "ambao hapana mtu atakayemwona Mungu asipokuwa nao." Waeb. 12:14. Neno lile husadikisha watu kuwa ni wenye dhambi, tena huonyesha njia ya kupata wokovu. Ni heri ulisikilize kama sauti ya Mungu inayosema nawe moyoni mwako.

Kama umefahamu dhambi jinsi ilivyo mbaya sana, na kujiona mwenyewe jinsi ulivyo katika hali ya kufanya dhambi, usikate tamaa. Kristo alikuja ili awaokoe wenye dhambi. Si juu yetu kufanya patanisho kati ya Mungu na sisi, lakini katika Kristo, Mungu mwenyewe alifanya patanisho. "Mungu alikuwa ndani ya Kristo, akiupatanisha ulimwengu na nafsi yake." 2 Wakor. 5:19. Hakuna hata mzazi wa kibinadamu ambaye angefanya saburi juu ya makosa ya mwanawe jinsi Mungu anavyofanya kwa wale atakao kuwaokoa. Ahadi zake zote, hata na maonyo yake yote, ni kwa ajili ya upendo wake tu, upendo usioelezeka hasa jinsi ulivyo.

Kama Shetani anakuambia kwamba wewe ni mwenye dhambi,
mwangalie Mwokozi wako na kuongea juu ya tabia na sifa zake. [38]

Ziungame dhambi zako na mwambie adui kwamba “Kristo Yesu alikuja ulimwenguni, awaokoe wenye dhambi.” 1 Tim. 1:15. Yesu alimwuliza Simon swali juu ya wadeni wawili. Mmoja alikuwa anamwia bwana wake pesa kidogo, na mwingine mapesa mengi, naye bwana yule aliwaachilia wote wawili; na Kristo akamwuliza Simon ni nani atakayempenda bwana wake zaidi. Simon alimjibu, “Nadhani ni yule aliyesamehewa naye mengi.” Luka 7:43.

Sisi tumekosa sana, lakini Kristo alikufa ili tupate kuachiliwa dhambi. Wale ambao amewaachilia zaidi, wao ndio watakaompenda zaidi na kukaa karibu naye, tena kumsifu zaidi katika ufalme wake kwa ajili ya upendo wake na dhabihu aliyoifanya kwa ajili yao.

Tukifahamu sana upendo wa Mungu jinsi ulivyo, ndipo tutakapozidi kufahamu dhambi jinsi ilivyo mbaya mno. Na jinsi tunavyozidi kufahamu kama Kristo alivyojinyima kwa ajili yetu, ndivyo tutakavyozidi kuchomwa moyo na kujitoa kwake kuwa watu wake kabisa.

## Sura 4—Kuungama Dhambi [39]

MWENYE kusetiri makosa yake hatasitawi: kila aziungamaye na kuziacha atarehemiwa." Methali 28:13.

Masharti yanayompasa mtu kufanya ili apate rehema ya Mungu si magumu, ni ya haki na ya maana. Bwana Mungu hataki tufanye mambo mazito ili tusamehewe dhambi; hasemi tufanye malipo makubwa kwa ajili ya dhambi zetu; asema tu kwamba anayeungama dhambi zake na kuziacha, ndiye atakayerehemiwa.

Mtume Yakobo asema, "Ungameni makosa yenu ninyi kwa ninyi, na kuombeana: mpate kuponywa." Yak. 5:16. Ungama dhambi zako hasa kwa Mungu, ambaye yeye tu ndiye awezaye kuzisamehe; lakini makosa ambayo umewafanyia wanadamu, basi uyaungame mbele ya wanadamu. Hivi ikiwa umemfanyia fulani yasiyofaa na kumchukiza kwa njia yo yote, nenda kwake na kuungama kosa lile ulilomfanyia, naye amepasiwa kulisamehe kabisa. Nyuma yake imekupasa kuomba msamaha kwa Mungu, kwa sababu huyo mwenzako ni kiumbe cha Mungu, na kumfanyia mwanadamu mako- sa ni kufanya makosa machoni pa Mungu pia. Hivyo kwa [40]
njia ya kuomba, mambo hufika mbele ya Mwombezi wetu, Kuhani Mkuu wetu ambaye "alijaribiwa sawasawa na sisi katika mambo yote, bila dhambi," naye awezaye "kuyachukua mambo yetu ya udhaifu," huweza kutusafisha uchafu wote wa dhambi.

Wale ambao hawajajishusha moyo mbele ya Mungu na kuziungama dhambi zao na kukiri kwamba wametiwa hatiani, hao nao hawajafanya bado jambo la kwanza lipasalo ili wapate kukubaliwa na Mungu. Isipokuwa tumemtubia Mungu kwa kweli, na kuchukizwa kabisa na maovu yetu, tumekuwa katika hali ya kutoomba kweli kwa kupata kusamehewa dhambi zetu; hivyo hatujapata kweli amani ya Mungu rohoni mwetu. Mtu akikiri dhambi zake, kukiri kwake lazima kuwa kwa moyoni; mtu akimtupia Mungu roho yake yote, Mungu atamhurumia kweli. "Bwana yuko karibu yao wenye moyo uliovunjika, wenye roho iliyopondeka huwaokoa." Zaburi 34:18.

Katika kuungama kwa kweli, imepasa kukiri dhambi au kosa hasa jinsi lilivyo. Pengine ni dhambi ambazo zimefaa kukiri wa kwa siri mbele ya Mungu tu; pengine ni tendo baya lifaalo kukiriwa kwa mtu mmoja tu, yule aliyehasiriwa kwa tendo lile; au pengine ni kosa lifaalo kukiriwa kwa wazi hadhara ya watu; hata ni dhambi au kosa
[41] la namna gani, mwenye kufanya kosa lazima kukiri kosa lile lile ambalo amelifanya.

Zamani wakati wa Samweli, Waisraeli walimwasi Mungu; tena waliona taabu kwa ajili ya dhambi zao. Walikuwa hawamwamini Mungu jinsi alivyokuwa na uwezo na akili kwa kuwatawala vizuri. Walimtupia Mfalme Mkubwa kisogo, nao walitaka kutawaliwa kwa jinsi yalivyotawaliwa mataifa mengine yaliyokuwa karibu nao. Na kabla ya kukubaliwa tena na Mungu, wakakiri hivi: "Tumeziongeza dhambi zetu kwa uovu wa kututakia mfalme." 1 Sam. 12:19. Kosa lile ambalo kwalo walitiwa hatiani, liliwalazimu kulikiri hasa.

Kukiri kutupu hakutakubaliwa na Mungu bila kutubu kwa kweli na kugeuka moyo na matendo na maisha; kila kitu kinachomchukiza Mungu lazima kutolewa ili mwenendo uwe safi machoni pake. Kazi iliyo wajibu wetu imeelezwa dhahiri hivi: "Osheni, safikeni; wekeeni mbali uovu wa matendo yenu toka machoni pangu; acheni kutenda maovu; jifunzeni kutenda mema; takeni hukumu, msaidieni mwenye kuonewa, mhukumieni yatima, mteteeni mjane." Isa. 1:16,17. "Mwovu atakaporudisha amana, akitoa tena aliyoitwaa kwa unyang'anyi, akiendea sheria za uzima, asipotenda maovu; kuishi ataishi hatakufa." Ezek. 33:15. Mtume Paulo alisema hivi juu ya ku-
[42] tubu: "Maana, angalieni, kuhuzunishwa kuko huko mbele za Mungu kwalitenda bidii ya namna gani ndani yenu: naam, na kujitetea, naam, na kukasirika, naam, na hofu, naam, na shauku, naam, na kujitahidi, naam, na kisasi. Kwa kila njia mmejionyesha kuwa safi katika jambo hilo." 2 Wakor. 7:11.

Kama maovu yametia giza macho ya kiroho, mwenye dhambi hawezi kutambua hali yake jinsi alivyo na upungufu, na jinsi makosa yake yanavyokuwa mabaya sana; tena isipokuwa atajitoa ili Roho Mtakatifu afanye kazi moyoni mwake, basi atadumu kuwa na giza la kiroho. Kukiri kwake si kwa kweli wala kwa haki. Anapoungama kosa lake hujisingizia akisema kwamba laiti mambo yasingalikuwa hivi na hivi, asingalifanya hivi na hivi, na hivyo asingalipata kukaripiwa.

Adamu na Hawa walipokwisha kula matunda yaliyokatazwa, waliona haya na hofu kuu. Mara ya kwanza walifikiri namna ya kujitetea kosa lao, ili waepukane na hukumu ya kifo. Mungu alipowauliza habari za kosa lao, Adamu akawa kama anamlaumu Mungu, akisema, "Mwanamke uliyenipa kuwa nami, ndiye aliyenipa ya mti, nikala." Yule mwanamke alimshtaki nyoka akisema, "'Nyoka alinidanganya, nikala." Mwanzo 3:12,13. Inaonekana kwamba wote wawili walikuwa wanamsingizia Mungu, Adamu kwa kuwa Mungu alimpa mwa- namke; tena Hawa kwa ajili ya kumwumba nyoka [43]
na kumwacha aingie katika bustani ya Aden. Ile roho ya kujifanya kuwa na haki ilianzishwa na yule baba wa uwongo, nayo huonekana kwa wanadamu wote. Kukiri namna hii na kujisingizia liaifai kitu, wala hakukubaliwi na Mungu. Katika kutubu na kukiri kwa kweli, mtu hukubali kwamba ametiwa hatiani bila kujisingizia wala kutaka kujifanya mwenye haki. Huomba kama yule mtoza ushuru alivyoomba, na kusema, "Mungu uniwie radhi mimi mwenye dhambi;" asitake hata kuinua macho yake mbinguni. Hao nao wanaokiri makosa yao kwa namna walivyotiwa hatiani, watapata msamaha, kwa kuwa Yesu atawaombea kwa ajili ya damu yake aliyomwagika kwao wenye kutubu.

Katika Neno la Mungu twasoma habari juu ya wengine wenye kutubu kwa kweli, na kujishusha mioyo na kuziungama dhambi, wala hawakuwa na moyo wa kujisingizia ama kujifanya wenye haki. Fikiri jinsi alivyosema Paulo, asitake kamwe kujiteteea makosa yake;"Niliwafunga wengi miongoni mwa watakatifu ndani ya magereza, nikiisha kupewa amri na makuhani wakuu; na walipouawa nalitoa. idhini yangu. Na mara nyingi katika masunagogi mengi naliwaadhibu, nikawashurutisha kukufuru; nikawaonea hasira kama nina wazimu, nikawaudhi hata katika miji ya ugenini." Matendo 26:10, 11. Lakini hakuogopa kusema, "Yesu Kristo alikuja [44]
ulimwenguni, awaokoe wenye dhambi; na mimi wa kwanza wao." 1 Tim. 1:15. Alijiona kuwa ni mwenye dhambi zaidi ya wengine wote.

Yule mnyenyekevu mwenye kupondeka moyo na kutubu kwa kweli, yeye atafahamu kidogo upendo wa Mungu, na dhabihu iliyofanywa Kalwari jinsi ilivyo na thamani kubwa sana. Tena jinsi mtoto atakavyoungama makosa yake mbele ya baba yake anayempenda, hivyo ndivyo mweye kutubn atakavyomletea Mungu dhambi

zake zote; kama ilivyoandikwa, "Tukiziungama dhambi zetu, yu amini na wa haki atuondolee dhambi zetu, na kutusafisha udhalimu wote. Yoh. 1:9

Ninaye Rafiki, naye alinipenda mbele;
Kwa kamba za pendo zake nimefungwa milele;
Aukaza moyo wangu, nisitengane naye:
Mimi wake, Yeye wangu; ndimi naye milele.

Ninaye Rafiki ndiye aliyenifilia;
Alimwaga damu yake kwa watu wote pia;
Sina kitu mimi tena, nikiwa navyo tele;
Pia vyote ni amana, ndimi wake milele.

Ninaye Rafiki, naye yuna na moyo mwema:
Ni Mlwalimu, Kiongozi, Mlinzi wa daima;
Ni nani wa kunitenga na Mepnzi wa mbele?
Kwake nimetia nanga, ndimi wake milele.

## Sura 5—Kujitoa Kuwa wa Mungu [45]

MUNGU ameahidi hivi: "Nanyi mtanitafuta, na kuona, mtakaponitafuta kwa moyo wenu wote." Yer. 29:13.

Isipokuwa moyo mzima umetolewa kuwa wa Mungu, mtu hawezi kugeuzwa kuwa katika hali ya kufanana na Mungu. Kwa hali yetu ya kibinadamu tumetengwa mbali na Mungu. Roho Mtakatifu ameeleza hali yetu kuwa ni hii: "wafu kwa sababu ya makosa yenu na dhambi zenu;" "kichwa chote kigonjwa, moyo wote umezimia;" "hamna uzima." Waef. 2:1; Isa. 1:5, 6. Mungu hutaka kutuponya na kutuweka huru. Kufanya hivyo ni kugeuza hali yetu kabisa, na kuifanya dhamiri yetu yote kuwa mpya; tena hayawezekani hayo ila sisi tukijitoa kabisa kuwa wake Mungu.

Kupigana kule ambako mtu hupigana na nafsi yake mwenyewe, ni vita vikubwa kuliko vyote. Kujitoa hivyo na kujisalimisha mkononi mwa Mungu, hakuwezekani bila mashindano moyoni; lakini isipokuwa mtu amejitoa na kujiweka chini ya mamlaka ya Mungu, hawezi kabisa kusafishwa na kuwa katika hali ya utakatifu. [46]

Mungu hawashurutishi watu wamtii, bila kwanza kuwaonyesha sababu ya maana yake, ili tupime kwa akili zetu jinsi ilivyo na kuchagua sisi wenyewe namna ya kufanya. "Njooni, tufanyane huja, asema Bwana." Isa. 1:18. Mungu halazimishi watu. Anataka tumtii na kumcha kwa hiari yetu wenyewe, si kwa lazima. Anataka tujitoe kwake sisi wenyewe, ili kwa Roho yake afanye kusudi lake mioyoni mwetu. Imekuwa juu yetu sisi kuchagua kwa hiari yetu ili tuondolewe katika utumwa wa dhambi, na kuwekwa huru kuwa wana wa Mungu.

Na pia, tukijitoa kwa Mungu, hivyo imetupasa kuacha vyote vinavyotaka kututenga mbali na Mungu. Mwokozi asema, "Kila mmoja wenu asiyeviacha vitu vyote alivyo navyo hawezi kuwa mwanafunzi wangu." Luka. 14:33. Hata jambo gani, liwalo lote, linalotuvuta macho kutoka kwa Mungu, lazima tuliache kabisa. Kupenda mali, kutaka fedha, ni kama minyororo inayofunga wengine kwa Shetani. Wengine hupenda sifa na heshima ya watu, na mambo

na anasa ya dunia. Imekuwa ni lazima kuikatakata minyororo hiyo yote. Hatuwezi kumpenda Mungu kwa moyo nusu, na nusu kuipenda dunia na mambo yake. Hatuwezi kuitwa watoto wa Mungu mpaka
[47] tutakapokuwa wake kabisa. Kuna wengine wanaosema kwamba wanamtumikia Mungu, na huku hujitegemea nguvu zao wenyewe kwa kufuata sheria za Mungu na kujipatia sifa njema na wokovu. Hawawi wakiamshwa mioyoni na kufahamu upendo wa Kristo kama inavyopasa; bali hujaribu kufuata mambo ya kikristo wakidhani kwamba kwa njia hiyo wataweza kujipatia mahali mbinguni. Dini ya namna hiyo haifai kitu.

Inapokuwa Kristo anakaa rnoyoni, roho inajaa upendo wake, hupenda kuongea naye, huambatana naye; hivyo pia mtu anajisahau nafsi yake kabisa na tamaa zake. Wale ambao hubidishwa moyoni kwa ajili ya upendo wa Kristo jinsi alivyojitoa kabisa kwa ajili yao, hawafikiri kumtii Mungu kwa kad ri ya kutosha kukubaliwa naye; bali hutaka kufikilia kile kipeo cha Kristo kwa kufuata matakwa yote ya Mwokozi wao.

Je, umeona ya kwamba kujitoa kwa Kristo ni kujinyima kupita kiasi? Jiulize hivi: "Kristo amefanya nini kwa ajili yangu?" Mwana wa Mungu alijitoa kabisa—maisha yake, kupendwa kwake, na kupata maumivu— ili apate kutukomboa. Na sisi je, wabaya wasiofaa kupendwa sana hivi, twawezaje kumkataa mioyoni mwetu? Tangu mwanzo wa maisha yetu tumepata mibaraka yake. Tungewezaje
[48] kumwangalia Yule aliyeumizwa kwa ajili ya dhambi zetu, na huku kutokubali upendo wake na dhabihu yake? Tukifikiri na kufahamu jinsi Yesu alivyojishusha kwa ajili yetu, sisi tungewezaje kunung'unika kupata uzima kwa njia ya kushindana na kujinyima na kujishusha mioyo?

Kosa la wengi wanaojisifu mioyoni mwao ni kusema hivi: "Mbona imenipasa kutubu na kujishusha moyo ili nijue kwa yakini kwamba nimekubaliwa na Mungu?" Mtazame Kristo. Yeye alikuwa mahali pasipo dhambi kabisa, tena zaidi ya hayo, alikuwa Mfalme wa mbinguni; lakini kwa ajili ya binadamu alihesabiwa kuwa ni mwenye dhambi. Alihesabiwa "pamoja na wakosao: ila dhambi za wengi akazichukua yeye, akawaombea wakosao. Isa. 53:12.

Lakini sisi je, hata tukijitoa kabisa kwa ajili ya Kristo, tumetoa nini? Moyo uliochafuka kwa dhambi, ili Yesu autengeneze na kuusafisha kwa damu yake, na kutuokoa kwa upendo wake mkuu.

Hata hivyo wanadamu huona kwamba ni vigumu kujitoa kwake kabisa. Kusema hivyo ni haya tupu.

Mungu hataki tuache kitucho chote ambacho kingekuwa na faida kwetu. Katika mambo yote, Mungu anataka tu ili tuwe na hali njema. Wote ambao hawajamchagua Kristo bado, laiti wangefahamu ya kwamba mambo ya dunia wanayoyataka, hayafai, kitu yakilinganishwa na vitu vizuri ambavyo Kristo anataka kuwapa. Yule afuataye [49]
njia iliyokatazwa na Mungu, hawezi kabisa kupata furaha ya kweli. Njia ya kufanya dhambi ni njia ya taabu na uharibifu.

Si vizuri kufikiri ya kwamba Mungu hupenda kuona watoto wake wakipata kuumizwa na kuona uchungu. Anataka ili watoto wake wapate furaha tu. Baba yetu aliye mbinguni anataka tuache kujaribu kujifurahisha na anasa za dunia, ambazo huleta maumivu na kulegea moyo kwa ajili ya kutopata raha na furaha jinsi inavyotazamiwa; na pia anasa zile zitatufungia mlango wa furaha ya mbinguni. Mwokozi hukubali watu jinsi walivyo, pamoja na mahitaji yao, upungufu wao, na udhaifu wao; tena pamoja na kuwasafisha moyo na kuwakomboa kwa damu yake, pia ataridhisha mioyo ya wote watakaomjia kwa ajili ya mkate wa uzima. Matakwa yake ni haya; tufanye mambo hayo tu yatakayotuongoza katika njia ya kweli, ili tufikilie kipeo cha furaha kisichoweza kufikiliwa na wale wasiomtii Mungu. Na kama Kristo anakaa ndani, hivyo ndivyo moyo huwa na furaha ya kweli.

Wengi wanauliza hivi: "Nawezaje kujitoa kwake Mungu?" Kweli umetaka kujitoa kwake, lakini umekuwa dhaifu katika dhamiri yako, una mashaka moyoni, umefungwa na mazoezi na matendo ya dhambi. Huwezi kutimiza ahadi na maazimio yako. [50]
Huwezi kutawala fikara zako, nia yako, wala mapenzi yako. Tena kama unafikiria hayo yote, unashuka moyo na kudhani ya kwamba hutakubaliwa na Mungu; lakini usikate tamaa. Jambo kubwa la kufahamu ni hili: Mungu ametupa sisi uwezo wa kuchagua kwa hiari zetu jinsi tutakavyofanya. Wewe mwenyewe huwezi kugeuza moyo wako; huwezi kwa nguvu zako mpaka Mungu upendo wa moyo wako; lakini waweza kuchagua kama unataka kumtii Mungu na kufanya mapenzi yake. Mpe nia yako na dhamiri yako ili apate kuitawala; ndipo Mungu atakapoweza kufanya kazi yako moyoni mwako, ili kutaka kwako na kutenda kwako kupatane na kusudi lake jema. Hivyo utajiweka chini ya mamlaka ya Kristo; upendo wako utavutwa kwake, utapatana na Kristo katika fikara zako.

Kutaka mema na usafi ni vizuri; lakini kutaka tu haifai kitu. Wengi watapotea wakiwa wanatamani tu kuwa Wakristo, kwa kuwa wanakosa kujiweka chini ya mamlaka ya Mungu katika dhamiri zao; huchelewa kuchagua kabisa ya kwamba watakuwa Wakristo sasa.

Ukitumia nia na dhamiri yako kwa njia ya kweli, hali ya maisha yako itageuka kabisa. Kama ukijiweka chini ya mamlaka ya Kristo,
[51] unajiunga na uwezo wa kupita uwezo mwingi- ne wo wote. Utakuwa na nguvu itokayo juu iwezayo kukuimarisha kabisa; tena kwa njia ya kujitoa na kujiweka chini ya mamlaka ya Mungu kila siku, utajaliwa kushi maisha mapya, maisha ya kumwamini Mungu daima.

Naendea msalaba, miye mnyonge na mpofu,
Yapitayo naacha, nipone msalabani.

Nakulilia sana: nalemewa na dhambi;
Pole Yesu asema: “Nitazifuta zote.

Natoa vyote kwako, nafasi nazo nguvu,
Roho yangu na mwili viwe vyako milele.

Kwa damu yake sasa nimegeuka roho,
Nikaziacha tamaa, nimtafute Yesu tu.

Nakutumaini tu, Ewe Mwana wa Mungu;
Nainamia kwako; niponye Mponya wangu.

Yesu yuaja tena! Nimepevuka kwake,
Kila chembe kamili; msifuni yeye Mponya.

# Sura 6—Kumwamini Mungu na Kukubaliwa Naye [52]

KWA jinsi dhamiri na roho yako vilivyohuishwa na Roho Mtakatifu, hivyo unazidi kufahamu ubaya wa dhambi, nguvu zake, na jinsi inavyoleta taabu; tena unazidi kuchukizwa nayo moyoni. Huona kwamba kwa ajili ya dhambi umepata kutengwa na Mungu, nawe umekuwa umefungwa na uovu. Huwezi kamwe kujisaidia mwenyewe. Nia yako si safi, tena moyo wako huwa najisi. Umefahamu kwamba maisha yako hujaa dhambi na mambo ya kujipendeza nafsi yako mwenyewe. Wataka sana kusamehewa makosa yako, ili upate kutakaswa na kuwekwa huru kutoka utumwa wa Shetani. Kupatana na Mungu, na kufanana naye, na kuwa salama moyoni,—waweza kufanya nini ili uwe katika hali hiyo?

Hali hii haiwezi kununuliwa kwa fedha, pia haipatikani kwa ajili ya akili wala elimu; tena huwezi kutumaini kuwa katika hali
hiyo kwa juhudi yako mwenyewe. Bali utaipata bure mkononi mwa [53]
Mungu kama karama yake, "pasipo fedha na pasipo thamani." Isa. 55:1. Ni juu yako tu kuichukua. Mungu asema, "Dhambi zenu zikiwa kama bendera (nyekundu), zitakuwa nyeupe kama theluji; zikiwa nyekundu nyekundu mno, zitakuwa kama sufu." Isa. 1:18. "Nami nitawapa ninyi moyo mpya, roho mpya nitatia ndani yenu." Ezek. 36:26.

Basi, umeziungama dhambi zako na kuziweka mbali na moyo wako. Pia umeazimia kujitoa kuwa mtu wa Mungu. Sasa nenda kwake, na kumwomba ili akusafishe dhambi zako zote, akupe moyo mpya. Ndipo usadiki kwamba amefanya hivyo *kwa kuwa ndivyo alivyoahidi*. Yesu alipokuwa hapa duniani, alitoa fundisho lile, kwamba imetulazimu kusadiki ya kuwa tumepata upaji wa Mungu aliotuahidi, *ndivyo utakavyokuwa wetu*. Yesu aliwaponya watu maradhi yao walipouamini uwezo wake. Aliwasaidia katika mambo waliyoweza kuyaona na macho ya kimwili, ili wapate kumtumainia juu ya mambo wasiyoweza kuyaona, yaani, wapate kusadiki uwezo wake katika kuwasamehe dhambi zao. Hivyo ndivyo alivyosema dhahiri katika kumponya yule mgonjwa wa kupooza: "*Ili mjue*

*ya kuwa Mwana wa Adamu ana mamlaka katika dunia kuondoa*
*dhambi*, (amwambia yule mgonjwa wa kupooza), Ondoka, ujitwike
[54] kita- nda chako, ukaende nyumbani kwako." Mattayo 9: 6. Mtume
Yohana pia, aliposema juu ya miujiza ya Kristo, alisema hivi: "Hizi
zimeandikwa mpate kuamini kwamba Yesu ni Kristo, Mwana wa
Mungu; na kwa kuamini mwe na uzima kwa jina lake." Yoh. 20: 31.

Hivyo tukisoma habari katika Biblia jinsi Yesu alivyoponya wagonjwa wa kimwili, twaweza kufundishwa na kufahamu namna ya kumsadiki kuwa kweli anaweza kuachilia na kuondoa dhambi. Tusome juu ya yule mgonjwa wa kupooza. Alikuwa hoi kwa ugonjwa tangu miaka thelathini na minane, asiweze kwenda kwa miguu. Walakini Yesu alimwambia, "Ondoka, ujitwike kitanda chako, ukaende." Yule mgonjwa angaliweza kusema: "Bwana, kama utaniponya, nitafanya usemavyo." Lakini sivyo. Alikubali neno la Kristo, alisadiki kwamba amepona, akajitahidi mara moja; alifanya jinsi Kristo alivyomwamuru, ndipo Mungu akamtolea nguvu zake, naye mgonjwa akapona mara, akawa mtu mzima.

Hivyo ndivyo ilivyo kwako mwenye dhambi. Huwezi kulipia
ukosefu wako, huwezi kugeuza moyo wako na kujitakasa mwenyewe
kuwa safi. Lakini Mungu ameahidi kwamba atakufanyia hivyo
katika Kristo. Unakubali hivyo? Na kwa jinsi unavyoziungama
dhambi zako, na kujitoa kwa Mungu na kuazimia kumtumikia, ndi-
[55] vyo Mungu atakavyotekeleza ahadi yake, nawe utaachiliwa dhambi
na kutakaswa; na utakuwa mtu mzima jinsi yule mgonjwa wa
kupooza alivyowezeshwa na Kristo kwenda kwa miguu mara ali-
posadiki kwamba amepona. Ikiwa unaamini kama yule, ndivyo
utakavyopata kupona katika dhambi.

Yesu asema, "Yo yote myaombayo mkisali, aminini ya kwamba mnayapokea, nayo yatakuwa yenu." Marko 11:24. Lakini kuna masharti juu yetu ili ahadi hii itimizwe,—tuombe kama vile apendavyo Mungu. Tena ni mapenzi ya Mungu kutuondolea dhambi zetu na kututakasa, ili tuwe watoto wake na kuishi maisha yaliyo safi kwa uwezo wake Mungu. Kwa hivyo twaweza kumwomba Mungu mibaraka hii, na kuamini kwamba tumeipata, na kumshukuru Mungu kwa kuwa kweli tumeipata mibaraka yake. Ni jambo linalotuhusu, kwenda kwake Yesu na kutakaswa, na kuhesabiwa kuwa ni safi bila lawama, na pasipo kuaibishwa "Sasa, basi, hapana hukumu juu

yao walio katika Kristo Yesu, wasioenenda kwa kufuata mambo ya mwili bali mambo ya Roho. "Warumi 8:1.

Toka sasa mwili wako si wako mwenyewe; umenunuliwa na bei kubwa. "Hamkukombolewa kwa vitu viharibikavyo, kwa fedha au dhahabu, . . . bali kwa damu ya thamani, kama ya mwana kondoo asiye na hila, na asiye na waa, ya Kristo, aliyejuliwa tangu zamani."
1 Petro 1: 18-20. Kwa kumwamini Mungu tu, Roho Mtakatifu [56]
ameanzisha, uzima mpya moyoni mwako. Sasa umekuwa kama mtoto aliyezaliwa kwa kiroho kuwa katika watu wa nyumba ya Mungu, naye anakupenda namna ampendavyo Mwana wake.

Sasa kama umejitoa kuwa wa Yesu, usirudi nyuma tena kutoka mkononi mwake. Kila siku heri useme, "Mimi ndimi wake Kristo; nimejitoa kwake;" tena umwombe Roho yake akulinde kwa neema yake. Ulipata kuwa mtoto wa Mungu kwa njia ya kujitoa kwake na kumwamini; hivyo ndivyo utakavyofanya kila siku ili uishi katika Kristo. "Basi, kama mlivyompokea Kristo Yesu, Bwana, enendeni vivyo hivyo katika yeye." Wakol. 2:6.

Wengine hufikiri kwamba ni lazima kuwa na wakati wa kujaribiwa na kumdhihirishia Mungu ya kuwa wameongoka kabla ya kuweza kupata mibaraka yake. Lakini sivyo. Waweza kupata mbaraka wa Mungu mara. Lazima wawe na Roho ya Kristo mioyoni mwao, kuwasaidia udhaifu wao katika kushindana na maovu. Yesu apenda ili tumwendee jinsi tulivyo,—wenye dhambi, wadhaifu, wasioweza kujiokoa wenyewe. Hata kama tumefanya mabaya ya namna gani, tusiogope kufika kwake. Atatupokea kwa moyo wa upendo, naye anakubali kututakasa makosa na unajisi wo wote.

Wengi huanguka katika neno hili; hawaamini kwamba Yesu
anawasamehe wao wenye- we hasa. Hawakubali ya kuwa jinsi [57]
Mungu asemavyo, ndivyo ilivyo. Ni haki ya watu wote wanaoyatimiza masharti ya Mungu, kujua kwa hakika kwamba kuna masamaha kwa kila dhambi. Ahadi za Mungu ni kwa kila mkosaji mwenye kutubu. Hata mwenye kufanya dhambi iwayo yote, hakuna asiyeweza kupata nguvu, na usafi, na kuwa mwenye haki katika Kristo Yesu aliyekufa kwa ajili yetu. Huwaambia waishi, na wasife.

Mungu hatutendei jinsi binadamu wanavyowatendea wenzao. Yu mwenye rehema, upendo, na huruma. Asema, "Aache mwovu njia yake, na mtu mbaya mawazo yake; akamrudie BWANA, naye atawarehemu; na kwa Mungu wetu, kwani mkarimu kuachilia."

“Nimefuta, kama wingu zito, makosa yako, na, kama wingu, dhambi zako.” Isa. 55:7; 44:22.

“Kwani sikifurahii kifo chake afaye, anena Bwana Mungu: basi geukeni, mkaishi.” Ezek. 18:32. Shetani yu tayari kila mara kutudanganya ya kwamba ahadi za Mungu si kwa watu kama sisi. Lakini tusisikilize maneno yake, bali tuseme hivi moyoni: Yesu alikufa kwa ajili yangu, niwe na uzima. Anipenda mimi; ataka nisife. Baba yangu aliye mbinguni ni mwenye huruma; na ingawa nimemtendea vibaya, na ingawa nimepoteza mibaraka yake kwa siku zilizopita, kwa vile anavyonipenda nitaondoka na kwenda
[58] kwa Baba na kusema, “Baba, nimekosa juu ya mbingu, na mbele yako; sistahili kuitwa mwana wako baada ya hayo; unifanye kuwa kama mmojawapo wa watumishi wako.” Mfano ule wa Mwana Mpotevu kuonyesha namna Mungu anavyowapokea wanaokuja kwake; “*Alipokuwa angali mbali*, baba yake akamwona, akamhurumia, akapiga mbio, akamwangukia shingoni, akambusu sana.” Luka 15: 18-20.

Na hata mfano huu umepungukiwa kuonyesha sawa namna ya upendo na huruma ya Baba aliye mbinguni, kwa kuwa huruma yake haina kifani. Mungu asema, *“Kupenda nimekupenda mapenzi ya milele; kwa hiyo na wema nimekuvutia.”* Yer. 31:3. Mwenye dhambi ingawa angali mbali na Baba yake, yule Babaanamhurumia moyoni mwake na kumtaka sana. Na kila mpotevu asikiaye moyoni mwake kwamba anataka kumrudia Mungu, ameona hivyo kwa kuwa Roho Mtakatifu anamvuta kwa Baba ampendaye sana.

Kama umezijua ahadi njema za Mungu zilizoandikwa katika Biblia, wawezaje kuona mashaka moyoni? Wawezaje kudhani kwamba Mungu angemkataa mwenye kumfikilia na kutubu? Fikara kama hizi ziondolewe mbali kabisa! Katika kumdhania Baba yetu hivi, unajihatarisha moyo wako mwenyewe. Ni kweli kama Mungu huchukizwa na maovu, lakini humpenda mwanadamu mpotevu, hata
[59] akajitoa pamoja na Kristo, ili aliye yote amwaminiye apate kuokoka na kurithi urithi wa milele katika ufalme wake mtukufu. Angeweza kusema nini tena zaidi ya hayo aliyoyasema kwa kuonyesha jinsi anavyotupenda sisi? Asema, “Aweza mwanamke kusahau mtoto wake anyonyaye, asimrehemu mwana wa tumbo lake? hata waweza hawa kusahau, ila siwezi mimi kukusahau wewe.” Isa. 49:15.

Inueni macho, ninyi mlio na mashaka na wenye kuogopa; Yesu ndiye Mwombezi wetu. Mshukuru Mungu kwa ajili ya Mwanawe Mpendwa, na kumwomba msaada wake ili isionekane kwamba kufa kwa Yesu kumekuwa bure kwako. Roho Mtakatifu anakuita hivi leo. Mtolee Yesu moyo wako mzima, ili upate mbaraka wake.

Nawe ukisoma ahadi zake, kumbuka kwamba yote husemwa kwa upendo na huruma. "Katika yeye tuna ukombozi kwa damu yake, masamaha ya dhambi kwa wingi wa neema yake." Waef. 1:7. Ndiyo, usadiki tu ya kuwa Mungu ni msaidizi wako. Anataka kuwarudisha wanadamu katika hali yao ya kwanza, kwa jinsi alivyowaumba kwa mfano wa Mungu. Nawe ukimkaribia Mungu na kuziungama dhambi zako na kutubu, yeye pia atakukaribia kwa moyo wa rehema na masamaha.

[60]

# KUMJUA YESU

Nitwae hivi nilivyo,
　　Umemwaga damu yako,
Nawe ulivyoniita,
　　Bwana Yesu, sasa naja.

　　Hivi nilivyo; si langu
Kujiosha roho yangu;
　　Nisamehe dhambi zangu,
Bwana Yesu, sasa naja.

Nawe hivi utanitwaa;
　　Nisisubutu kukawa,
Na wewe hutanikataa,
　　Bwana Yesu, sasa naja.

　　Hivi nilivyo; mapenzi
Yamenipa njia wazi;
　　Hali na mali sisazi,
Bwana Yesu, sasa naja.

## Sura 7—Dalili ya Kuwa Wanafunzi wa Kristo [61]

MTU akiwa ndani ya Kristo, ni kiumbe kipya; vya kale vimepita; kumbe! vyote vimekuwa vipya.” 2 Wakor. 5:17.

Pengine mtu hawezi kutaja siku wala mahali hasa alipoongoka kuwa mfuasi wa Kristo; lakini kukosa kufanya hivyo si kama kusema kwamba yule hakuongoka kweli. Kristo alimwambia Nikodemo, “Upepo huenda utakako, na sauti yake waisikia, lakini hujui unakotoka wala unakokwenda; kadhalika na kila mtu aliyezaliwa kwa Roho.” Yoh. 3:8. Upepo hauwezi kuonekana, lakini twasikia na kuona matendo yake; na vilevile Roho ya Mungu inajulikana kwa namna ya matendo yake mioyoni mwa wanadamu. Uwezo wake, usionekane na macho ya kibinadamu, huanzisha maisha mapya moyoni; humwumba mtu kuwa mpya kwa mfano wa Mungu. Ijapokuwa kazi ya Roho inatendeka kwa kimya, tena haionekani; matokeo yake yamekuwa waziwazi. Kama Roho Mtakatifu ametengeneza moyo kuwa mpya, jambo hilo litaonekana katika maisha yake aliyeongoka [62] moyo. Ingawa sisi wenyewe hatuwezi kugeuza mioyo yetu, ama kuzifanyiza nia zetu kupatana na Mungu; tena haifai kabisa kujitegemea wenyewe kwa matendo yetu yaliyo mema; walakini, kwa namna ya maisha yetu, itajulikana kama tunayo neema ya Mungu mioyoni mwetu. Itaonekana kwamba tabia zetu, desturi zetu, mazoea yetu, na mambo yetu yote yamegeuka kuwa mbalimbali na yale ya zamani. Tabia na desturi za mtu fulani zinajulikana si kwa matendo mema au mabaya ya siku moja moja tu, ila kwa maelekezo ya matendo yake na maneno yake, na mazoea yake ya siku zote.

Ni kweli ya kuwa kuna watu ambao mienendo yao ni myema machoni pa wenzao, bila kuongoka moyo kwa ajili ya Kristo. Kwa sababu ya kupenda kusifiwa na kuwa kama waongozi kati ya wengine, hivyo hujilinda ili waonekane kuwa ni wenye adabu. Kwa ajili ya kujistahi nafsi zao, huyaepuka matendo mabaya ya nje. Hata mwenye kuzoea kujifikiria nafsi yake mwenyewe na kujipendeza, pengine anafanya mema. Ikiwa ni hivyo, twawezaje kuyakinisha kama tumekuwa upande wa Kristo, au sivyo?

Ni nani anayeutawala moyo? Fikara zetu ni juu ya nini? Tuna-
[63] zoea kuzungumza juu ya nani? Ni nani ambaye tunampenda zaidi na kumtumikia? Ikiwa tu watu wa Kristo, fikara zetu ni juu yake. Tunajitoa kwake pamoja na vyote tulivyo navyo. Twataka kufanana naye, kuwa na Roho yake mioyoni, kufanya mapenzi yake na kumpendeza kwa mambo yote.

Wale wanaokuwa wapya katika Kristo Yesu, hao nao watazaa matunda ya Roho, yaani, "upendo, furaha, amani, uvumilivu, utu wema, fadhili, uaminifu, upole, kiasi." Wagal. 5:22, 23. Hawatafuata tamaa zao za zamani, bali watamwamini Mwana wa Mungu na kufuata nyayo zake; tabia zake zitaonekana katika maisha yao, watatakaswa kuwa safi kama yeye alivyo mtakatifu. Mambo waliyochukizwa nayo zamani, sasa wanayapenda; na vile walivyopenda zamani, sasa huchukizwa navyo. Yule aliyefanya kiburi, sasa huwa mpole na mnyenyekevu. Mlevi huacha ulevi wake, mwasherati na mzinzi huachana na matendo yao ya zamani, na kuwa watu safi. Mkristo hafuati anasa na mvao na mambo ya kidunia. Hataki kufanana na watu wa dunia kwa "kujipamba kwa nje," "ila mtu wa moyoni asiyeonekana, katika jambo lisiloharibika; ni roho ya upole na utulivu iliyo ya thamani kuu mbele ya Mungu." 1 Petro 3:3, 4.

Toba si ya kweli isipokuwa imeonekana dhahiri kwamba mtu huongoka moyo na kufanya yaliyo mema. Kama mtu anarudisha
[64] amana yake, na kutoa tena aliyoitwaa kwa unyang'anyi, kuziungama dhambi zake, kumpenda Mungu na wenziwe, yule aliye mwenye dhambi anaweza kutumaini kwamba "amepita toka mauti hata uzima." Yoh. 5:24.

Sisi wanadamu ambao tungali wabaya, tukimfikilia Kristo na kupata kusamehewa dhambi zetu, hali yetu inageuka kabisa. Upendo huonekana moyoni. Twapata furaha katika kufanya yaliyo wajibu wetu sisi Wakristo; twapenda kujinyima kwa ajili yake Kristo. Zamani tulikuwa gizani, na sasa tuko katika nuru yake aliye "Jua la haki."

Tabia za Kristo zitaonekana katika wafuasi wake. Yeye alijitoa kufanya mapenzi ya Mungu kwa kuwa alimpenda Mungu. Mungu ni upendo. Upendo wa kweli hutoka kwa Mungu; pia unapatikana katika moyo ule tu ambao Yesu huutawala. Haupatikani kamwe katika moyo usioongoka na kujitoa kuwa wa Mungu. "Sisi twapenda kwa maana yeye kwanza alitupenda sisi." 1 Yoh. 4:19. Upendo

wa Mungu ukiwa humo mioyoni mwetu, maisha yetu yatakuwa safi, hata wengine katika jirani zetu watavutwa moyo na kutaka kutengeneza maisha yao kuwa safi, hasa kwa ajili ya mfano mwema wao walio Wakristo wema.

Kuna makosa mawili ambayo watu wa Mungu hawana budi [65]
kujihadhari nayo. La kwanza, kujitumainia matendo mema yao wenyewe ili wapatane na Mungu. Hakuna awezaye kujitakasa mwenyewe ila kwa njia ya kuamini neema na msaada wa Kristo.

Kosa la pili litupasalo sisi kuwa na hadhari nalo ni kinyume cha lile la kwanza, ndilo kufikiri kwamba hatuna haja kuzishika sheria za Mungu; wengine hufikiri ya kuwa kama tumewekwa haki kwa neema ya Kristo tu, basi hakuna inayotakiwa juu yetu ili tupate wokovu katika Kristo. Lakini sivyo kabisa.

Angalia ya kwamba kumtii Mungu siyo kwa matendo ya nje yanayoonekana tu, bali kwa mambo ya moyo na upendo. Kumpenda Mungu ni asili ya kumtii. Mwanadamu awapo na upendo moyoni na kuwa katika mfano wa Yule aliyemwumba, ndipo inapotimizwa ahadi ya Agano Jipya ya Mungu jinsi inavyoandikwa, "Nitatia sheria zangu mioyoni mwao, na katika akili zao nitaziandika." Waeb. 10:16. Na sheria ikiwamo moyoni, itakuwa inaongoza katika mambo yote ya maisha ya mwanadamu. Kumtii Mungu kwa sababu ya kumpenda, hiyo ndiyo dalili ya kweli kama mtu fulani ni mfuasi wake, Imeandikwa hivi katika Biblia, "Huku ndiko kumpenda Mungu, kuzishika amri zake." "yeye asemaye, Nimemjua, naye hazishiki amri zake, ni mwongo, na kweli haimo ndani yake. 1
Yoh. 5:3;2:4, Hivyo twaona ya kwamba imetakiwa ili tumtii Mungu [66]
na kuzishika amri zake; lakini kwa kumwamini Kristo tu tutaweza kumtii kwa njia ya kweli.

Hatuwezi kustahili wokovu kwa ajili ya utii wetu; wokovu ni thawabu ya Mungu iliyotolewa bure, nasi tunaipokea kwa kumwamini Mungu. Na kumtii Mungu hufuatana na kumwamini. "Mnajua ya kuwa yeye alidhihiri ili aziondoe dhambi zetu; na dhambi haimo ndani yake. Kila akaaye ndani yake hatendi dhambi; kila atendaye dhambi hakumwona, wala hakumtambua." 1 Yoh. 3:5, 6. Hiyo ndiyo dalili ya kweli inayodhihirisha kama mwanadamu ni mfuasi wa Kristo. Kama tunakaa ndani ya Kristo, na upendo wa Mungu hukaa mioyoni mwetu, ndipo mawazo na matendo yetu yatakapopatana na mapenzi ya Mungu jinsi yanavyonenwa katika

amri zake takatifu. “Wanangu, mtu asikudanganyeni; afanyaye haki yuna haki; kama yeye alivyo na haki.” 1 Yoh. 3:7. Namna ya haki inayotakiwa na Mungu imeelezwa kwa kipimo cha sheria yake, jinsi inavyonenwa katika zile amri kumi zilizotolewa na Mungu katika mlima wa Sinai.

Kusema ya kuwa tunamwamini Kristo, na huku kusema kwamba hatuna haja kumtii Mungu kwa mambo ya amri zake, hiyo si kuamini kwa kweli, bali ni kama kufanya kiburi tu, maana “mmeokolewa
[67] kwa neema, kwa njia ya imani.” Waef. 2:8. Lakini “imani isipokuwa na matendo, imekufa nafsini mwake.” Yak. 2:17. Na Yesu, kabla ya kuja kwake duniani, alisema, “Kufanya mapensi yako, Ee Mungu wangu, ndio furaha yangu; na sheria yako imo ndani ya moyo wangu.” Zab. 40:8. Tena kabla ya kurudi kwake mbinguni alisema, “Mkizishika amri zangu, mtakaa katika pendo langu; kama mimi nilivyozishika amri za Baba yangu, na kukaa katika pendo lake.” Yoh. 15:10. Tena katika Maandiko imeandikwa hivi: “Na hivi twajua ya kuwa tumemjua, ikiwa tunashika amri zake. . . Hivi twajua ya kuwa tumo ndani yake. Yeye asemaye ya kuwa anakaa ndani yake, imempasa kuenenda mwenyewe vilevile kama yeye alivyoenenda.” “Maana Kristo naye aliteswa kwa ajili yenu, akiwaachieni mfano, mfuate nyayo zake.” 1 Yoh. 2:3-6; 1 Petro 2:21.

Sharti la kupata uzima wa milele limekuwa moja tangu zamani,—jinsi lilivyokuwa katika bustani ya Aden kabla Adamu na Hawa hawajaanguka na kufanya dhambi,—ndilo hili, kumtii Mungu kwa ukamilifu katika mambo yote ya amri zake, kuwa na haki kamilifu katika Kristo. Sisi peke yetu hatuna haki kabisa, ila kwa Kristo tu. Yesu alikaa hapa duniani, akajaribiwa kama sisi. Akaishi maisha yaliyo makamilifu pasipo dhambi. Akafa kwa ajili yetu; akajitoa
[68] badala yetu; alikubali kuzichu- kua dhambi zetu ili sisi tupate kupewa haki kwake. Kama unajitoa kwake, ua kumkubali kuwa ni Mwokozi wako, ijapokuwa umekuwa mwenye dhambi kabisa, utahesabiwa kuwa mwenye haki katika Kristo. Sifa njema ya Kristo itahesabiwa kuwa ni yako, nawe utakuwa katika hali ya kukubaliwa na Mungu kana kwamba hukufanya dhambi kabisa.

Zaidi ya hayo, Kristo huigeuza hali ya moyo jinsi ilivyo. Hukaa ndani ya moyo wako kwa njia ya kuamini. Nawe imekupasa kuendelea kumwamini Kristo na kumtolea nia yako siku zote ili upate kumshiriki Kristo daima; na kwa kadiri unavyoendelea kufanya

hivyo, ndivyo atakavyotenda kazi ndani yako, ili kutaka kwako na kutenda kwako vipatane na kusudi lake jema. Ndipo utaweza kusema, "Uhai nilio nasa katika mwili, ninao katika imani ya Mwana wa Mungu aliyenipenda akajitoa nafsi yake kwa ajili yangu." Wagal. 2:20. Ndivyo Kristo alivyowaambia wanafunzi wake: "Kwa kuwa si ninyi msemao, bali Roho ya Baba yenu asemaye ndani yenu." Mattayo 10:20. Na kama Kristo atenda kazi ndani yako, utakuwa na nia sawa na nia iliyokuwamo ndani ya Kristo na kutenda matendo kama vile alivyotenda yeye—matendo yaliyo ya kaki, na kumtii Mungu.

Basi, hatuna kitu chema ndani yetu cha kujisifu nacho. Hatuna
sababu ya kujitukuza. Tumaini letu pekee ni katika haki ya Kristo: [69]
ya kwamba itahesabiwa kwetu kama ni yetu wenyewe: tena katika haki hiyo, ikitendeka ndani yetu kwa kazi ya Roho Mtakatifu.

Tukisema juu ya imani, lazima tufahamu ya kwamba kuna tofauti kati ya kusadiki tu ya kuwa Mungu yu hai, na kumwamini kabisa katika moyo. Hata Shetani na malaika wabaya huamini ya kuwa Mungu yuko; huamini uwezo wake, na maneno yake jinsi yalivyo ya kweli: ni mambo wasiyoweza kuyakana. Biblia inasema, "Mashetani nao waamini na kutetemeka," Yak. 2:19; lakini hiyo siyo imani ya kweli. Mwarninifu wa kweli hujitoa kabisa kuwa wa Mungu na kufanya mapenzi yake. Kwa imani ya kweli moyo unatengenezwa kuwa mpya kwa mfano wa Mungu. Moyo na nia ya mwili, iliyo katika hali ya zamani, haitii sheria ya Mungu wala haiwezi; bali yule aliyeongoka moyo, sasa hupata furaha katika amri zake, na kusema "Nimeipendaje sheria yako! Ndio fikara yangu mchana kuchwa." Zab. 119:97. Na hivyo "wema uagizwao na torati unatimizwa ndani yetu," tusioenenda "kwa kufuata mambo ya mwili, bali mambo ya roho." Warumi 8:4,1.

Kuna wengine ambao wamejua upendo wa Kristo na jinsi anavyowasamehe dhambi zao, nao wanataka sana kuwa watoto wa Mungu;
walakini wanaona ya kwamba sifa yao si kamili, na maisha yao [70]
si sawa. Hao wamekaribia kuona shaka kama kweli mioyo yao imefanywa mipya na Roho Mtakatifu. Na wote wa namna hiyo nawaambia hivi: Msife moyo ninyi, wala kurudi nyuma. Mara kwa mara tutalazimishwa kumwendea Yesu tukihuzunika kwa ajili ya makosa yetu; lakini haifai kushushwa moyo. Ingawa tumeshindwa na adui, Mungu hatatuacha na kututupilia mbali. Sivyo; mtume

Yohana aliandika, “Na ijapo mtu akatenda dhambi, tuna Mwombezi kwa Baba, Yesu Kaisto mwenye haki.” 1 Yoh. 2:1. Tena tusisahau maneno yake Kristo: “Baba mwenyewe awapenda ninyi.” Yoh. 16:27. Mungu anataka kukurudisha kwake mwenyewe, na kuona mfano wake ndani yako jinsi Yeye alivyo safi na mtakatifu. Endelea kuomba kwa moyo wa bidii zaidi; na kumwamini Mungu kabisa. Na kwa jinsi tunavyopungua kujitegemea uwezo wetu wenyewe, tuzidi kutegemea na kutumainia uwezo wa Mwokozi wetu na kumsifu.

Na kwa vile unavyozidi kumkaribia Yesu, hivyo utazidi kujiona mwenyewe kuwa u mwenye makosa zaidi; kwa kuwa macho ya kiroho yatazidi kuwa safi ya kufahamu namna ya ukosefu na upungufu wako, kwa vile unavyomtazama Yesu na kujilinganisha naye jinsi alivyo mkamilifu.

[71] Mtu asiyefahamu hali yake jinsi alivyo mbaya na mwenye dhambi, yule hawezi kumpenda Yesu sana moyoni mwake; bali yule ambaye ameongoka moyo kwa neema ya Kristo, yeye atamheshimu Kristo kwaajili ya sifa yake njema. Lakini isipokuwa tumefahamu hali yetu katika dhambi, tunabainisha ya kwamba hatujaona bado uzuri na ubora wa Kristo.

Kwa jinsi tunavyopungua kujiona tu bora wenyewe, ndivyo tutakavyozidi kumheshimu Mwokozi wetu kwa wema na utakatifu wake. Mtu anapofahamu udhaifu wake na kumtaka Kristo, Kristo naye atamsaidia na kumjulisha uwezo wake. Na kwa vile tunavyozidi kuona ubora na sifa ya Kristo, ndivyo tutakavyozidi kuwa katika mfano wake.

Yesu kwetu ni Rafiki, hwambia haja pia;
  Tukiomba kwa Babaye, maombi asikia;
Lakini twajikosesha, twajitweka vibaya;
  Kwamba tulimwomba Mungu, dua angesikia.

  Una dhiki na maonjo? Una mashaka pia?
Haifai kufa moyo, dua atasikia.
  Hakuna mwingine M wema, wa kutuhurumia;
Atujua tu dhaifu; maombi asikia.

Je, hunayo hata nguvu, huwezi kwendelea,
  Uja podharauliwa, ujaporushwa pia.

Watu wangekudharau, wapendao dunia,
    Hukwambata mikononi, dua atasikia.

    Bwana Yesu unitazame sasa,
Unifanye niwe dhabihu hai;
    Najitoa kwako, moyo, na vyote
Unioshe sasa niwe mweupe.

[72] # Sura 8—Kukua Katika Kristo na Kuwa Watu Wake Wakamilifu

KULE kuongoka moyo ambako kunatufanya tupate kuwa watoto wa Mungu, kumenenwa katika Biblia kama ni kuzaliwa. Pengine tena kumelinganishwa na kuota kwa mbegu njema zilizopandwa na mlimaji. Vivyo hivyo wale ambao wameongoka moyo na kuanza kumfuata Kristo ni kama "watoto wachanga," ( 1 Petro 2:2 ), tena lazima wakue hata wawe kama watu wazima katika Kristo Yesu. Kadiri zinavyotakiwa mbegu njema kwa mimea mizuri, basi pia imewapasa watu wawe na mbegu njema moyoni ili watoe matunda mema ya kiroho. Isaya asema juu yao, "Wapate kuitwa miti ya haki, miche ya BWANA, atukuzwe." Isa. 61:3.

Akili zote na ustadi wote wa binadamu haviwezi kamwe kuhuisha kitu cho chote ulimwenguni. Hata wanyama wala mimea, vyote hupata kuhuishwa na Mungu tu. Hivyo wanadamu hawapati kuzaliwa mara pili na kupata uzima mpya wa kiroho ila katika uzima
[73] utokao kwa Mungu. Mtu asipozaliwa mara ya pili, hawezi kushiriki uzima ule ambao hutolewa na Kristo.

Na jinsi ilivyo katika kupata uzima, ndivyo ilivyo katika kuendelea kukua. Mimea haipati maua na matunda yake ila kwa uwezo wa Mungu tu. Yeye ndiye anayeziotesha na kukuza mbegu, "kwanza jani, tena suke, kisha ngano pevu katika suke," Marko 4:28. Mimea haikui kwa kuhangaika kujitahidi yenyewe, ila kwa kuvipokea vile inavyopewa na Mungu kwa kuendesha uzima wake. Hivyo pia mtoto hawezi kuongeza urefu wake kwa kujitahidi mwenyewe. Na wewe pia, kwa kujishughulisha na kuhangaika kwako huwezi kuendelea kukua katika mambo ya kiroho. Mmea au mtoto hupata kukua wakipokea vile vinavyoweza kusaidia na kuendesha uzima wao,—hewa, na chakula. Na kwa kadiri vitu vile vinavyosaidia kwa kuendesha uzima wa sasa, ndivyo alivyo Kristo kwa wale waaminifu wake. Yeye ndiye "nuru ya milele" kwao, "ndiye jua na ngao." (Isa. 60:19; Zab. 84:11). "Atakuwa kama umande kwa Israel." "Atashuka kama mvua juu ya majani yaliyokatwa." ( Hosea 15:5, Zab. 72:6 ).

Yeye ndiye maji ya uzima, "mkate wa Mungu . . . ushukao kutoka mbinguni na kuupa ulimwengu uzima. Yoh. 4:14; 6:35,33.

Yesu mwenyewe hufundisha mambo haya haya anaposema, [74]
"Kaeni ndani yangu na mimi ndani yenu. Kama vile tawi lisivyoweza kuzaa peke yake, lisipokaa ndani ya mzabibu, kadhalika na ninyi, msipokaa ndani yangu . . . Maana pasipo mimi hamwezi kufanya neno." Yoh. 15:4,5. Tawi lazima lifungamane na mti wenyewe ili lipate kukua na kuzaa matunda; basi, wewe pia imekulazimu kumtegemea Kristo ili upate kuishi maisha safi. Pasipo yeye huna uzima kabisa. Peke yako huwezikuyakinga majaribu, wala kukua kwa namna ya kiroho na kuwa mtu mwenye usafi. Unapokaa ndani yake utasitawi. Kama unaishi kwake, huwezi kunyauka wala kutozaa matunda. Bali utakuwa kama mti uliopandwa mtoni penye maji.

Wengi hudhani kwamba ni wajibu wao kufanya sehemu ya kazi ile wenyewe. Wamemtumainia Kristo kwa kusamehewa dhambi, lakini sasa wanaona ya kwamba ni heri wajitahidi wenyewe ili waishi maisha yaliyo sawa. Kujitahidi hivyo hakutafaulu kamwe. Yesu asema, "Pasipo mimi hamwezi kufanya neno." Tena ni kwa njia ya kushiriki naye na kuongea naye, kwa kukaa ndani yake kila siku saa zote, tunavyopata kukua kwa namna ya kiroho. Yeye si mwanzo tu wa imani yetu, ila mwisho wake pia; yaani, imetupasa kumtumainia Kristo tangu mwanzo mpaka mwisho. Imetupasa ili Kristo akae nasi, siyo tu kwa siku zile tuanzapo kumjua na siku za mwisho wa
maisha yetu, ilakini kwa mwenendo wetu wote katika maisha yetu [75]
yote. Daudi alisema, "Nimeweka BWANA siku zote mbele yangu: kwa sababu yuko mkono wangu wa kuume, sitatikisika." Zab. 16: 8.

Pengine unauliza, Nawezaje kukaa ndani ya Kristo?" Kama vile ulivyompokea moyoni mara ya kwanza. "Kama mlivyompokea Kristo Yesu, Bwana, enendeni vivyo hivyo katika yeye." "Mwenye haki ataishi kwa imani." Wakol. 2:6; Waeb. 10:38. Ulijitoa kwa Mungu kuwa mtu wake kabisa, kumtii na kumtumikia tena ulimtumaini Kristo kama Mwokozi wako. Wewe mwenyewe hukuweza kujiondolea dhambi zako na kugeuza moyo wako; lakini ulipokuwa umejitoa kuwa wa Mungu, ndipo uliposadiki kama Mungu ndiye aliyekutendea haya yote kwa ajili ya Kristo. Kwa njia ya *kumwamini Kristo*, ulikuwa wake; tena kwa kumwamini hivyo utazidi kukua naye—kwa kujitoa na kumpokea. Lazima *ujitoe kwake kabisa*,—

moyo wako, nia yako, na utumishi wako; jitoe kwake na kuzishika amri zake na matakwa yake yote. Hivyo pia *imekupasa kuvipokea vyote* vinavyotoka kwa Kristo, ili akuwezeshe kumtii sawa sawa; umkubali Kristo mwenye mibaraka yote akae moyoni mwako, awe uwezo wako, na haki yako, na msaidizi wako daima.

[76] Jitoe kwake Mungu kila asubuhi, kabla hujafanya kitu cho chote. Omba hivi: "Bwana wangu, unichukue, niwe wako kamili. Nia yangu na maazimio yangu yote nayaweka mbele yako. Unitumie leo, niwe mtumishi wako. Ukae nami ili kazi yangu yote itendeke kwa uwezo." Hili ni jambo lipasalo kwa kila asubuhi, kujitoa kuwa wa Mungu kwa siku ile. Makusudi yote na miradi yako yote uweke mbele yake ili kuyafanya au kutofaya kwajinsi atakavyokuonyesha. Hivyo ndivyo maisha yako yatakavyokuwa mkononi mwa Mungu kila siku, na maisha yako yatazidi kuwa kwa mfano wa Kristo.

Kukaa ndani ya Kristo ni kukaa raha mustarehe moyoni, na kutulizwa roho. Matumaini yako si juu yako mwenyewe, ila kwa Kristo. Udhaifu wako umefungamana na ujinga wako na kutojua kwako hufungamana na akili zake, na nguvu zake, uhafifu wako umefungamana na uwezo wake. Hivyo haifai kujiangalia nafsi na kujiwazia sana; yapasa kumwangalia Kristo tu, na kufikiri sana juu ya upendo wake na sifa yake jinsi ilivyo njema na timilifu. Jinsi Kristo alivyojinyima, na udhilifu wake jinsi alivyoaibishwa, jinsi alivyo safi na mtakatifu, upendo wake usio na kifani,—hayo ndiyo mambo vafaayo kufikiriwa moyoni. Kwa njia ya kumpenda Yesu, kumfuatisha kwa namna ya matendo yake na tabia zake, kumtegemea na kumtumainia kabisa, utapata kugeuka kuwa katika mfano wake.

[77] Yesu asema, "Kaeni ndani yangu." Maneno haya yatufikirisha juu ya kukaa mustarehe na imara, na kuwa na matumaini. Asema tena, "Njooni kwangu, nami nitawapumzisha." Mattayo 11:28,29. Mtunga Zaburi alisema hivi: "Umnyamalie BWANA, ukamngoje." Zab. 37:7. Na Isaya pia hutuambia, "Kwa kunyamaza na kutumaini zitakuwa nguvu zenu." Isaya. 30:15. Kustarehe huku hakupatikani kwa kukaa bure katika hali ya kutofanya kazi; kwa kuwa katika maneno yale ya Mwokozi wetu, ahadi ya kupata raha imeungamana na wito wa kufanya kazi. "Jitieni nira yangu, . . . nanyi mtapata raha." Mattayo 11:29. Yule anayemtegemea Kristo zaidi na kukaa

raha kwake moyoni, ndiye atakayekuwa mtu wa moyo na juhudi kwa kumtumikia Mungu.

Kama mtu anajifikiria nafsi na kujipendeza mwenyewe tu, roho yake hugeuka na kutoka kwa Kristo ambaye ni uwezo na uzima wake. Kwa hivyo Shetani huwa anafanya bidii kuvuta watu na kuwapotosha, ili kuwazuia wasimshiriki Kristo. Anasa za dunia, fadhaa na mashaka, na ama huzuni, makosa ya wengine, makosa na upungufu wako mwenyewe—Shetani hutumia hayo yote kwa kupotosha fikara za watu. Tujiangalie tusidanganywe na hila zake. Wengi wanaotaka kufanya yapasayo na kuishi maisha safi machoni pa Mungu, mara nyingi huvutwa kwa Shetani katika kufikiri sana [78]
juu ya makosa yao na udhaifu wao mpaka wamejitenga mbali na Kristo. Tusifikiri nafsi zetu sana, na kuhangaika na mashaka moyoni kama tutaokoka au sivyo. Mambo kama hayo hugeuza moyo kutoka kwa Kristo aliye asili ya nguvu zetu. Weka roho yako mkononi mwa Mungu kama amana, na kumtumainia. Mazungumzo yako na fikara zako ziwe juu ya Yesu. Usiwe na shaka wala hofu moyoni. Serna kama alivyosema mtume Paulo: "Ni hai; wala si mimi tena, bali Kristo yu hai ndani yangu; na uhai nilio nao sasa katika mwili, ninao katika imani ya Mwana wa Mungu aliyenipenda akajitoa nafsi yake kwa ajili yangu." Wagal. 2:20. Ukae na kustarehe kwa Mungu, ukasadiki kwamba aweza kukilinda kile ulichokiweka amana kwake. Kama unajiweka mkononi mwake, atakuwezesha kushinda, na zaidi ya kushinda, kwa yeye aliyekupenda. ( Soma Warumi 8:37).

Kristo alipoutwaa mwili wa kibinadamu, alijifungia mioyo ya wanadamu kwake kwa upendo wake, na kufungamana huku hakuwezi kuharibika ila kwa hiari ya mwanadamu mwenyewe. Shetani hufanya bidii siku zote kuvuta roho zetu na kutushawishi ili tujitenge mbali na Kristo. Kwa hivyo imetupasa kujilinda, na kuomba kwa bidii ili tusishawishiwe na jambo lo lote na kuchagua kutawaliwa na Shetani. Tumkazie Kristo macho yetu, yeye [79]
awezaye kutulinda. Tukimtazama Yesu, tutakuwa salama; wala hakuna awezaye kutupokonya katika mkono wake. Tukimwangalia Yesu na utukufu wake daima, "tunabadilishwa na kufananishwa na mfano huo huo, toka utukufu hata utukufu, kama vile kwa utukufu utokao kwa Bwana aliye Roho." 2 Wakor. 3:18.

Hivyo ndivyo wanafunzi wake wa zamani walivyopata kufanana naye. Walikuwa naye wakafundishwa kwake. Wakamwangalia,

kama watumishi wanavyomwangalia bwana wao, ili wapate kujua yaliyo wajibu wao. Walikuwa wanadamu wenye "tabia moja na sisi." Yak. 5:17. Wakawa wakishindana na maovu sawa na sisi. Iliwapasa kusaidiwa kama sisi, ili wapate kuishi maisha yaliyo safi na matakatifu.

Na hata Yohana, mwanafunzi mpendwa wa Yesu, aliyefanana naye zaidi ya wengine, hakuwa na sifa njema kwa desturi. Alikuwa mtu wa kujitokeza mbele na kutaka makuu. Naye alipozidi kufahamu namna ya sifa ya Yesu jinsi ilivyo bora, alizidi kuona upungufu wake mwenyewe na kushushwa moyo. Siku kwa siku moyo wake ukazidi kuvutwa kwa Yesu Kristo, na kujisahau nafsi yake mwenyewe. Moyo wake ulitengenezwa kuwa mpya kwa Roho Mtakatifu, na hata tabia zake hasa zaligeuka kufanana na Kristo.
[80] Hivyo ndivyo itakavyokuwa kwa kila ashirikianaye naYesu. Kristo akaapo ndani ya moyo, na kuutawala, ndipo yule mwanadamu anapogeuzwa tabia zake hasa; sasa fikara zake na tamaa zake ni juu ya Mungu na mambo ya mbinguni.

Siku ya kupaa kwake mbinguni, Yesu aliwaambia wanafunzi wake, "Tazama, mimi nipo pamoja nanyi siku zote, hata mwisho wa dunia." Mattayo 28:20. Akapaa mbinguni na umbo la kibinadamu. Walijua ya kwamba alikwenda kuwaandalia makao, na kurudi tena baadaye, kuwapeleka kwake alipo.

Walipokutana walikumbuka ahadi yake jinsi alivyosema, "Mkimwomba Baba neno kwa jina langu atawapeni. Mpaka leo hamkuomba neno kwa jina langu; ombeni, na mtapata, furaha yenu iwe timilifu." Yoh. 16:23,24. Pia walitumaini ya kwamba "Kristo ndiye aliyekufa, naam, na zaidi ya haya, amefufuka, naye yuko mkono wa kuume wa Mungu, tena ndiye anayetuombea." Warumi 8:34. Na siku ya Pentekote wakapata kujazwa Roho Mtakatifu, yule Mfariji ambaye Kristo ailsema juu yake, "Naye atakaa ndani yenu." Alisema pia, "Yawafaa ninyi niondoke; kwa maana nisipoondoka, Mfariji hatakuja kwenu; bali nikienda zangu, nitampeleka kwenu." Yoh. 14:17; 16:7. Tangu siku hiyo, kwa njia ya Roho Mtakatifu, Kristo amekuwa anaweza kukaa mioyoni mwa watu wake siku zote,
[81] Sasa waweza kumshiriki Kristo zaidi kuliko walivyomshiriki siku zile alipokuwa nao katika umbo la kibinadamu. Upendo na uwezo wa Kristo vikaonekana kwao, hata wengine walipotambua hivyo,

"wakastaajabu, wakawatambua ya kwamba walikuwa pamoja na Yesu." Matendo 4:13.

Kwa kadiri Kristo alivyowasaidia wanafunzi wake wa zamani, ndivyo apendavyo kuwasaidia watu wake wa sasa; kwa kuwa katika kuomba kwake alisem. "Wala si hao tu ninaowaombea, bali na wao watakaoniamini kwa sababu ya neno lao." Yoh. 17:20.

Yesu alituombea sisi, ili tuwe katika umoja ndani yake, kama Yeye na Baba yake walivyo katika umoja. Huo ni umoja wa namna gani! Mwokozi alisema juu yake mwenyewe, "Mwana hawezi kutenda neno kwa nafsi yake, ila lile amwonalo Baba analitenda;" akasema tena, "Baba akaaye ndani yangu huzifanya kazi zake." Yoh. 5:19; 14:10. Ikiwa Kristo anakaa mioyoni mwetu, atatenda kazi yake ndani yetu, ili kutaka kwetu na kutenda kwetu kupatane na kusudi lake jema.Wafil. 2:13. Tutafanya kama alivyofanya yeye; tutakuwa na nia ndani yetu iliyokuwamo ndani yake; hivyo kwa kumpenda Yesu na kukaa ndani yake, tutakua "mpaka tumfikie yeye katika yote, aliye kichwa, ndiye Kristo. Waef. 4:15.

[82] 

## KUMJUA YESU

Fuaha gani na ushiriki
    Nikimtegemea Yesu tu!
Baraka gani, tena amani,
    Nikimtegemea Yesu tu!

    Tegemea,
Salama bila hatari;
    Tegemea,
Tegemea Bwana Yesu tu.

Nitaiweza njia nyembamba,
    Nikimtegemea Yesu tu;
Njia ‘tazidi kuwa rahisi,
    Nikimtgemea Yesu tu.

    Sina sababu ya kuogopa,
Nikimtegemea Yesu;
    Atakuwa karibu daima,
Nikimtegemea Yesu tu.

## Sura 9—Kazi na Maisha, Jinsi Vinavyohusiana [83]

MUNGU ndiye asili ya uzima na mwanga na furaha kwa ulimwengu wote. Mibaraka inatoka kwake kwa viumbe vyake vyote. Na mahali po pote ukiwapo uzima wa Mungu mioyoni mwa wanadamu, itakuwa kama mito ya maji ya uzima ule, kuwatokea na kuwasaidia na kuwabariki wengine.

Ilikuwa furaha ya Mwokozi wetu kuwainua na kuwakomboa wanadamu wapotevu. Kwa hiyo hakuyahesabu maisha yake kuwa ni kitu cha thamani kwake, lakini "kwa ajili ya furaha iliyowekwa mbele yake aliuvumilia msalaba na kuidharau aibu." Waeb. 12:2. Hivyo pia malaika hushughulika katika kazi ya kufurahisha wengine. Hiyo ndiyo furaha yao. Kazi ile ambayo wengine hudhani ni kazi ya namna ya kuwavunjia heshima na cheo, yaani kuwahudumia na kuwasaidia walio chini yao na wenye hali mbaya, ndiyo kazi wanayoifanya malaika wakaao mahali pasipo dhambi kabisa. Ile nia ya Kristo ya kutojipendeza nafsi yake, bali kufikiria na kusaidia [84]
wengine, ndiyo nia inayoenea kote mbinguni, tena ni asili ya furaha yao wa mbinguni. Hiyo ndiyo nia watakayokuwa nayo wafuasi wa Kristo, na namna ya kazi watakayoifanya.

Upendo wa Kristo ukiwamo moyoni, hauwezi kufunikika, bali utatambulika kwa wote tunaokutana nao. Kumpenda Yesu kutabainishwa katika kutamani kutenda kama alivyotenda yeye, kwa kusaidia na kubariki walimwengu wengine. Tutakuwa na moyo wa upendo, na huruma, na kushiriki katika hali ya wengine wote walio viumbe vya Baba yetu aliye mbinguni.

Mwokozi alipokuwa hapa duniani, hakukaa raha mustarehe na kujipendeza mwenyewe; bali alifanya bidii kuwaokoa wanadamu wapotevu. Tangu kuzaliwa kwake mpaka kusulubiwa kwake Kalwari, alifuata njia ya kujinyima. Alisema ya kwamba Mwana wa Adamu hakuja "kuhudumiwa, bali kuhudumu, na kutoa roho yake kuwa dia ya wengi." Mattayo 20:28. Hilo ndilo kusudi kuu la maisha yake, kufanya mapenzi ya Mungu na kumaliza kazi yake. Hakufikiri kamwe juu ya kujipendeza nafsi yake mwenyewe.

Vivyo hivyo wale wanaomshiriki Kristo watakuwa tayari kujinyima ili wengine wapate kujua jinsi Yesu alivyokufa kwa ajili
[85] yao, nao pia washirikiane naye. Hiyo ndiyo roho inaooynekana kwa yule anayeongoka kweli. Mara anapomjua Kristo, husikia moyoni kwamba ameshurutishwa kuwajulisha wengine kuwa Yesu ni rafiki wake mwema. Ikiwa tumesikia wema wa Bwana wetu, basi, tuwaonyeshe wenzetu, ili wao pia wavutwe kwa Yesu, na kumjua "Mwana Kondoo wa Mungu, aichukuaye dhambi ya ulimwengu." Yoh. 1:29.

Tukijitahidi hivyo kusaidia wengine tutabarikiwa sisi pia. Mungu alikusudia hivi alipotupa sisi sehemu ya kazi ya kuokoa watu. Kuwa watenda kazi pamoja na Mungu ni heshima iliyo kuu na furaha iliyo kubwa zaidi ya yote wanayoweza wanadamu kupewa na Mungu.

Mungu angaliweza kuwapa malaika kazi ya kuwahubiria wanadamu Injili. Lakini kwa upendo wake alituchagua tuwe watenda kazi pamoja naye, pamoja na Kristo na malaika, ili tushiriki mibaraka, furaha, na kuchangamshwa roho kwa jinsi inavyopatikana katika huduma hii. Tena kila tendo la kujinyima kwa kuwasaidia wengine, humzidishia moyo wa ukarimu yule mwenye kujinyima, naye huzidi kupatana na kushirikiana na Mwokozi; "maana mmejua neema ya Bwana wetu Yesu Kristo, jinsi alivyokuwa maskini kwa ajili yetu, alipokuwa tajiri, ili ninyi mpate kuwa matajiri kwa umaskini wake." 2 Wakor. 8:9. Tena kwa kadiri tunavyotimiza kusudi
[86] la Mungu juu yetu, ndivyo tutakavyopata furaha na baraka katika maisha yetu.

Kama utafanya kazi kama Kristo alivyokusudia wafuasi wake wafanye, na kuwavuta watu kwake, utaona haja ya kuzidi kumjua Mungu moyoni mwako, na kuzidisha maarifa katika mambo ya Mungu, nawe utaona "njaa na kiu ya haki." Utaendelea kumwomba Mungu, tena kuamini kwako kutazidi kuthibitika. Kama unapata kujaribiwa utashurutishwa kusoma Neno la Mungu na kumwomba zaidi. Hivyo utazidi kumjua Kristo, na kupata neema yake na kuwa mwaminifu wake katika maisha yako; hasa utazidi kufanana na Kristo, tena utapata raha na furaha zaidi moyoni mwako.

Wale wanaojaribu kuwa Wakirsto na kupata mibaraka yake bila kumfanyia kazi yo yote, hufanana na watu wanaotaka kupata chakula na kukaa bure bila kufanya kazi. Mtu anayekataa kuvinyosha viungo

vyake kwa kutenda kazi, atapotewa na nguvu ile aliyo nayo. Vivyo hivyo Mkristo anayekataa kuutumia uwezo ule aliopewa na Mungu, hukosa kukua na kuwa kama mtu mzima katika Kristo, hata na yeye pia atapotewa na uwezo wa kiroho aliokuwa nao zamani.

Mungu ameweka kanisa la Kristo kuwa kama wakili wake kwa kuwaokoa watu. Kazi yake: ni kueneza Injili duniani pote. Sharti
hiyo imekuwa juu ya Wakristo wote. Kama tumejua upendo wa [87]
Kristo, basi tunawiwa deni na wote wasiomjua Kristo. Mungu ametupa nuru, si kwa kujisaidia sisi wenyewe tu, ila pia tumulikie wale wengine wasiomjua.

Wafuasi wa Kristo wangaliamka na kufanya wajibu wao, kungekuwako watu elfu wa kuhubiri Injili mahali palipo na mhubiri mmoja tu sasa. Na hata wale wasioweza wenyewe kuwa watenda kazi wa Mungu, wangesaidia kazi kwa fedha zao na maombi yao. Tena kazi ya kueneza Injili na kuwajulisha watu kuwa Kristo ndiye Mwokozi wao, ingeendelea na kufanywa kwa moyo wa bidii sana.

Si lazima twende katika nchi ngeni za makafiri, kumfanyia Kristo kazi, ikiwa wajibu wetu uko huko kwetu. Twaweza kumtumikia Kristo nyumbani mwetu, kanisani kwetu, kwa wenzetu, majirani zetu, hata na wale tunaokutana nao katika kazi yetu.

Katika maisha yake hapa duniani, Yesu alipitisha miaka mingi katika kufanya kazi ya useremala pamoja na babake mjini Nazareti. Tena alimwamini Mungu katika kufanya kazi ile kama alivyokuwa akiwaponya wagonjwa na kutembea juu ya maji ya Galilaya. Hivyo na sisi pia, hata ikiwa tumehesabiwa kuwa tu watu duni na kufanya kazi iliyo chini, twaweza kutembea na Yesu na kumtumikia.

Mtume Paulo asema, "Kila mtu . . . na akae katika hali hiyo hiyo [88]
aliyoitwa." 1 Wakor. 7:24. Mfanyi biashara anaweza kufanya kazi yake kwa namna awezavyo kumtukuza Mungu kwa ajili ya uaminifu wake. Ikiwa yu mfuasi wa kweli wa Kristo, dini yake itaonekana katika mambo yake yote, na atawadhihirishia watu namna ya roho ya Kristo. Mwashi, au mfanyi kazi yo yote, inampasa kuwa mwenye bidii tena mwaminifu katika kazi yake, na hivyo atakuwa mjumbe mwaminifu wa Kristo. Kila mtu anayejiita kwa jina la Kristo inampasa kutenda kazi kwa namna iliyo sawa, ili wengine wapate kuyaona matendo yake mema wakamtukuze Mungu aliye Muumba tena Mwokozi wetu.

Wengi hujisingizia wasitumie akili zao katika kufanya kazi ya Kristo, kwa sababu kuna watu wengine wanayo akili iliyo bora zaidi. Watu wengi hudhani ya kwamba wale tuwenye akili nyingi ndio ambao wametakiwa kujitoa na akili zao katika kumtumikia Mungu. Pia wengi hudhani ya kwamba ni baadhi tu va watu, yaani wanaopendelewa zaidi na kuwa Katika hali nzuri, ambao hupewa akili na talanta; na wengine wametengwa mbali, hao nao hawapati kutiwa kushiriki kazi ya Mungu na neema yake. Lakini haikuelezwa hivyo katika mfano uliotolewa na Kristo. Bwana wa nyumba alipowaita watumishi wake, alimpa kila *mmoja kazi yake*.

[89] Kwa moyo wa kupenda, twaweza kuifanya hata kazi iliyo chini kabisa na kuifanya "kama kwa Bwana." Wakol.3:23. Upendo wa Mungu ukiwamo moyoni, utaonekana katika maisha.

Usingojee jambo lililo kuu wala kutumaini kupata akili nyingi kabla ya kumtumikia Mungu. Tena usifikiri juu ya wengine jinsi watakavyokudhania. Kama maisha yako na matendo yako ya siku zote huushuhudia wema wako na uaminifu wako, na kuwasadikisha wengine ya kwamba unataka kuwatendea valiyo mema, kazi yako haitapotea bure. Hata na wafuasi wa Yesu wanaohesabiwa kuwa ni watu duni, wanaweza kusaidia wengine na kuwaletea baraka. Kama wanaendelea kufanya kwa uaminifu kazi ile wanayopewa na Mungu, maisha yao hayatakuwa bure. Watazidi kufanana na Kristo mioyoni mwao; huwa wafanyi kazi pamoja na Mungu katika maisha ya sasa, na vivyo hivyo wanatayarishwa kumhudumia Mungu mbinguni, na kupata furaha kuu katika uzima ujao.

## Sura 10—Kumjua Mungu [90]

KWA njia nyingi Mungu anajaribu kutujulisha tabia zake, ili tupate kumjua na kushirikiana naye. Viumbe vya ulimwengu vyatuonyesha wema na upendo wake milele. Moyo unaofunuliwa utaona upendo na utukufu wa Mungu jinsi unavyoonekana katika matendo yake na katika kazi za mikono yake. Tukiona na kufikiri juu ya miti na maua, mazao ya mashamba, mawingu, mvua, mito, nyota na uzuri wote wa mbingu, hatuna budi kuvutwa moyoni kumjua yeye aliyeviumba vyote.

Mwokozi wetu alitoa mafundisho mengi juu ya viumbe vya ulimwengu. Akasema juu ya miti, maua, ndege, vilima, maziwa ya maji, na vitu vya mbinguni, pamoja na mambo yanayotukia kwa watu katika maisha yao siku zote; na watu walipoviona vitu vile na mambo hayo mara kwa mara iliwalazimu kukumbuka mafundisho yake.

Tukifunua roho zetu na kusikiliza sauti ya Mungu katika viumbe vyake, tutapata kufundishwa namna ya kumtii na kutawakali kwa Mungu. Viumbe vyote, tangu nyota zinazofuata njia zao mbin- [91]
guni, hata na vidudu vidogo, vyote hufuata mapenzi ya Mungu. Tena Mungu huangalia kila kitu alichokiumba. Huzitegemeza nyota katika mahali pakubwa mbinguni, na hata ndege wadogo wa anga huangaliwa naye. Wanadamu wakiondoka asubuhi kwenda kazini, na wakati waombapo, wakati wanapokwenda kulala usiku; tajiri katika jumba lake, hata na maskini katika kibanda chake, Baba yetu aliye mbinguni huangalia wote kwa huruma na upendo. Mtu akitoka machozi ama akiwa na furaha, Mungu huona yote.

Kama tungesadiki hivyo kabisa, mahangaiko yote yasiyofaa yangeondolewa mioyoni mwetu; kwa sababu mambo yote, makubwa hata madogo, tungekuwa tunayaacha mkononi mwa Mungu; nasi tungeona raha mioyoni mwetu.

Na kama unapendezwa machoni kwa kuona uzuri wa dunia hii, fikiri juu ya ulimwengu mpya ujao, ambao huko uharibifu wa dhambi na mauti hautaonekana kamwe. Tena ukumbuke ya kwamba

fahari yake na utukufu wake havina kifani. Imeandikwa, "Mambo ambayo jicho halikuyaona wala sikio halikuyasikia, wala hayakuingia katika moyo wa kibinadamu, mambo ambayo Mungu aliwaandalia wampendao." 1 Wakor. 2:9. Wale tu watapata furaha katika
[92] kutambua uzuri wa viumbe vya ulimwengu, ambao wanafahamu ya kwamba vyote hutangaza upendo wa Mungu kwa wanadamu.

Mungu husema nasi katika matendo yake, pia katika uongozi wake, tena katika mvuto wa Roho yake mioyoni mwetu. Katika mambo yanayotukia kwetu, na katika hali yetu, twaweza kupata mafundisho yake, ikiwa mioyo yetu imekuwa wazi kuyatambua mafundisho yu Mungu. Mtungu Zaburi alisema, "Nchi imejaa wema wa Bwana." "Mwenye hekima utayaangalia haya, nao watazijua rehema za Bwana." Zaburi 33:5; 107:43.

Mungu husema nasi tena katika Neno lake. Hapo imefunuliwa dhahiri sana namna ya sifa zake na tabia zake, jinsi anavyowatendea wanadamu, na kazi yake kubwa katika kuwakomboa wanadamu. Hapo zimesimuliwa habari za wazee wakuu na manabii na wengine wa zamani waliokuwa watu wa Mungu. Hao nao wakawa watu wenye "tabia moja na sisi." Yakobo 5:17. Twasoma juu yao jinsi walivyoshindana na mambo ya kulegeza moyo kama sisi tunavyolazimishwa kushindana; walijaribiwa na kuvutwa na mabaya kama sisi tunavyopata kuvutwa; hata hivyo walijitia moyo tena, wakashinda kwa uwezo na neema ya Mungu; na sisi pia tukijua hivyo imetupasa kujitia moyo na kuendelea kujitahidi katika kuyanyosha maisha yetu
[93] ili yawe na haki ma- choni pa Mungu. Kama tunaona namna ya kazi ya wale watu wa zamani waliyofanya kwa neema na msaada wa Mungu, na jinsi walivyobarikiwa na kupata furaha katika kufanya kazi ile, sisi pia twatamani kufanana nao katika sifa zao na kuendelea pamoja na Mungu kama wao.

Maandiko Matakatifu hutoa habari za Kristo, jinsi alivyosema, "na hayo ndiyo yanayonishuhudia." Yoh. 5:39. Biblia nzima hutoa habari za Kristo. Tangu habari za mwanzo juu ya kuumbwa kwa ulimwengu kwa kuwa "pasipo yeye hakikufanyika cho chote kilichofanyika," Yoh. 1:3—mpaka ahadi ya mwisho, "Angalieni, naja upesi," Uf. 22:12, twasoma juu ya matendo yake tena twasikiliza sauti yake. Kama unataka kumjua yule aliye Mwokozi, heri ufanye bidii katika kuyachunguza maneno ya Biblia, yaani Maandiko Matakatifu.

Ujaze moyo mzima maneno ya Mungu. Hayo ndiyo maji ya uzima, na mkate wa uzima utokao juu. Yesu alisema, "Msipoila nyama yake Mwana wa Adamu na kuinywa damu yake, hamna uzima ndani yenu." Akazidi kueleza maana yake hivi: "Maneno ninayowaambieni ni roho, tena ni uzima." Yoh. 6:53, 63. Kadiri miili yetu inavyokuwa mizima na kupata afya njema kwa ajili ya
vile tulavyo na tunywavyo, basi vivyo hali yetu ya kiroho itazidi [94]
kuwa njema na kuongezeka nguvu kwa vile tunavyofikiri na kuwaza mambo ya kiroho.

Jambo la ukombozi wa watu katika Kristo ndilo jambo ambalo malaika wanatamani kulichungulia; tena litakuwa jambo kuu katika kuelimisha wateule wa Mungu katika ufalme wake hata milele. Je, si jambo lifaalo kufikiriwa hata na sisi katika siku hizi? Imetupasa kufikiri sana juu ya rehema na upendo wa Yesu, na jinsi alivyojitoa maisha yake kwa ajili yetu. Imetupasa kuchunguza sifa na tabia za Mwokozi wetu. Ni wajibu wetu kufikiria kazi yake katika kuwaokoa watu katika dhambi zao. Na tunapowaza mambo matakatifu, imani yetu na upendo wetu vitaongezeka kwake, tena kwa hiyo maombi yetu yatazidi kukubaliwa na Mungu. Tutazidi kumtegemea na kumtumainia Kristo na uwezo wake "kuwaokoa kabisa wao wajao kwa Mungu kwa yeye." Waeb. 7:25.

Na tunapofikiri juu ya Mwokozi jinsi alivyo mkamilifu na mwenye sifa bora, tutatamani kugeuka moyo kuwa wapya na hufanana naye hasa katika usafi wake. Tena tukizidi kumfikiria Kristo, tutazidi kumshuhudia kwa wengine.

Biblia haikuandikwa kwa ajili ya wenye elimu nyingi tu; bali ilikusudiwa kuwa ya watu wote, hata na akina sisi. Mafundisho
makubwa juu ya wokovu yamekuwa dhahiri kabisa, na mtu ye yote [95]
aweza kuyafahamu; hakuna awezaye kukosa njia ya haki ila yeye afuataye nia yake mwenyewe badala ya kufuata mapenzi ya Mungu.

Tusikubali neno lo lote la binadamu juu ya mafundisho ya Biblia, bali tujifunze wenyewe maneno ya Mungu na kuyachunguza hata tufahamu maana yake. Tukifanya bidii katika kujifunza mambo ya Biblia, tukilinganisha sehemu fulani ya Biblia na sehemu nyingine, na mambo ya kiroho, kwa mambo tutaona ya kuwa akili zetu zinaongezeka.

Hakuna njia nyingine ya kuzidisha akili zaidi ila ya kujifunza na kuyachunguza maneno ya Biblia. Mafundisho yake yaweza

kuadilisha fikara na kuzidisha akili kwa namna isiyowezekana kwa kusoma kitabu kingine cho chote.

Kama wanadamu wangejifunza na kulichunguza Neno la Mungu kama inavyostahili, wangekuwa na maarifa mengi na sifa bora, na kuimarishwa mioyoni.

Lakini hakuna faida katika kusoma Biblia ovyo ovyo kwa haraka. Kwa kusoma namna hiyo tungeweza kuisoma Biblia nzima bila kutambua uzuri wake wala kufahamu maana yake, hasa maana ya siri ya ndani. Yafaa kuisoma sehemu moja na kuichunguza sana mpaka maana yake imekuwa dhahiri, na kuona jinsi inavyohusiana na mpango wa Mungu kwa kuwaokoa wanadamu; kufanya hivyo
[96] kwa kila sehemu ya Biblia kutakuwa na faida sana kuliko kusoma tu sura nyingi bila kusudi la kujifunza hakika yake. Biblia yako iwe karibu nawe kila mara. Kila upatapo nafasi, isome; jifunze mafungu yake kwa moyo. Hata wakati utembeapo, waweza kulisoma fungu fulani na kufikiri maana yake, na kulitia moyoni.

Hatuwezi kupata kuelimishwa bila kujitahidi na kukaza moyo kwa kujizoeza kusoma pamoja na kuomba. Kuna sehemu nyingi za Biblia ambazo maana yake imekuwa dhahiri kabisa; lakini kuna sehemu zingine tena ambazo maana yake si rahisi kufahamiwa mara moja. Yafaa kulinganisha sehemu moja na sehemu nyingine, na kuzifikiri na kuzichungua sana pamoja na kuomba. Tusifungue kabisa Biblia na kuyasoma maneno yake bila kuomba. Kabla ya kuifungua Biblia heri tusali ili tupate mwangaza wa Roho Mtakatifu, ndipo tutaupata. Nathanael alipomwendea Yesu, Mwokozi alisema, "Tazama, huyu ni Mwisraeli kweli kweli, hamna hila ndani yake." Nathanael akamwambia, "Umepataje kunijua?" Yesu akamjibu, "Kabla Filipo hajakuita, ulipokuwa chini ya mtini, nalikuona." Yoh. 1:47, 48. Tena Yesu ataonana nasi katika mahali pa siri pa sala, ikiwa tutamwomba ili tupate kuelimishwa na kujua yaliyo ya kweli. Malaika watokao mbinguni watawasaidia wale watakao kuongozwa na Mungu.

[97] Roho Mtakatifu humtukuza na kumsifu Mwokozi. Kazi yake ni kutuonyesha Kristo, na hali yake jinsi ilivyo yenye haki na usati, na kutudhihirishia habari za wokovu tupatao kwake. Yesu alisema, "Atatwaa katika iliyo yangu, atawapasheni habari." Yohana 16:14. Roho ya kweli ndiye mwalimu wa pekee awezaye kutujulisha barabara yaliyo kweli ya Mungu. Ni dhahiri ya kwamba Mungu

huona wanadamu kuwa wa thamani kubwa, kwa kuwa alimkubali Mwanawe afe kwa ajili yetu, tena ameweka Roho wake Mtakatifu kuwa mwalimu na kiongozi wa wanadamu daima.

Nataka nimjue Yesu,
    Na nizidi kumfahamu;
Nijue pendo lake, na
    Wokofu wake kamili.

    Nataka nimwone Yesu,
Na nizidi kusikia
    Anenapo kitabuni,
Kujidhihirisha kwangu.

Nataka nifahamu, na
    Nizidi kupambanua
Mapenzi yake, nifanye
    Yale yanayompendeza.

    Nataka nikae naye,
Kwa mazungumzo zaidi,
    Nizidi kuwaonyesha
Wengine wokofu wake.

[98]

## Sura 11—Kuomba ni Faradhi Yetu

MUNGU hutumia njia nyingi kwa kusema nasi, yaani kwa viumbe vyake, kwa kuwafunulia wanadamu mambo yajayo, kwa maongozi yake, na kwa mvuto wa Roho yake Mtakatifu. Lakini hata njia hizi zote hazitoshi; hata na sisi pia imetupasa kumtolea Mungu yote yaliyomo mioyoni mwetu. Imetulazimu kuongea na Baba yetu aliye m binguni, ili tupate uzima na nguvu za kiroho. Na kama twataka kuongea na Mungu, sharti tuwe na mambo ya kumwambia, hasa juu ya maisha yetu.

Katika kuomba tunamfunulia Mungu mioyo yetu na kuongea naye kama tunavyoongea na rafiki wa kweli. Si lazima kufanya hivyo ili kumjulisha Mungu hali yetu ilivyo, bali kuongea naye kunatuwezesha kumpokea mioyoni mwetu. Sala hazimlazimishi Mungu kushuka kwetu, bali ni sisi ambao tunainuliwa mpaka kufika kwake.

Yesu alipokuwa hapa duniani, aliwafundisha wanafunzi wake kusali. Aliwaagiza waweke mbele ya Mungu upungufu wao na
[99] mahitaji yao ya kila siku, na kumtupia mashaka yao na mahangaiko yao yote. Tena kama alivyowaahidi wanafunzi wake ya kwamba maombi yao yatakubaliwa, basi ahadi ile imekuwa yetu pia; yaani anatuahidi ya kuwa sala zetu zitakubaliwa.

Yesu mwenyewe, alipokaa na wanadamu, aliomba kwa kawaida. Mwokozi wetu alijishirikisha mahitaji yetu na udhaifu wetu; kwa hivi akawa mhitaji na mwombaji, akimwomba Baba yake ili apate nguvu za kufanya kazi yake na kuyashinda majaribu yatakayompata. Yeye ndiye mfano wetu katika mambo yote. Ni ndugu yetu ashirikiye udhaifu wetu, "alijaribiwa sawa sawa na sisi katika mambo yote;" lakini kwa sababu alikuwa safi bila dhambi, akayaepuka maovu nafsini mwake. Katika hali yake ya kibinadamu, kuomba kulikuwa ni faradhi yake iliyomhusu, naye tena akapata faraja na furaha katika kuongea na Baba yake. Na ikiwa Mwokozi wetu, aliye Mwana wa Mungu, aliona ya kwamba anahitaji kuomba, basi sisi, tulio wanadamu dhaifu wenye dhambi, tunahitaji zaidi

kufanya bidii katika maombi ya kawaida. Baba yetu aliye mbinguni huwa anangoja kutubariki. Mungu yu tayari kusikiliza maombi ya kweli ya kila mtoto wake, walakini sisi hatuna moyo sana wa kumwambia Mungu haja zetu.

Giza ya Shetani huzunguka wale wasiofanya bidii katika [100]
kuomba. Adui wao, Shetani, huwashawishi ili wafanye maovu, nao kwa sababu ya kuacha kuomba hawana nguvu za kushindana naye. Mbona watu wa Mungu hutupilia mbali faradhi yao ya kuomba, ijapokuwa kuomba ni kama ufunguo mikononi mwa waaminifu wa Mungu wa kuwafungulia msaada wote na mibaraka yote ya Mungu isiyo na kiasi. Tusipoomba siku zote na kukesha kwa uangalifu, tutajitia katika hatari ya kuwa walegevu wa mambo ya kiroho na kupotewa na njia ya haki.

Kuna masharti mengine juu yetu ambayo ni wajibu wetu, ili tuweze kutumaini ya kuwa Mungu atatusikia na kutujibu maombi yetu. Shart moja ni hili; lazima tufahamu jinsi tunavyohitaji msaada wake. Ameahidi, "Nitamimina maji juu yake mwenye kiu, na mito juu ya pakavu." Isa. 44:3. Wale wenye njaa na kiu ya haki, wamtakao Mungu sana, watashiba. Lakini baraka za Mungu haziwezi kupatikana ila kwanza moyo uwe umefunguliwa na Roho Mtakatifu kuingia. Bwana wetu hujua haja zetu, lakini imetupasa kutambua haja zetu sisi wenyewe na kumwomba Mungu mambo hayo. Asema, "Ombeni na mtapewa." Mattayo 7:7. Tena "Yeye asiyemwachilia Mwana wake yeye, bali alimtoa kwa ajili yetu sisi sote. atakosaje kutukarimia na vitu vyote pamoja naye?" Warumi 8:32.

Tukiwa tunaangalia maovu moyoni na kuyashikilia, Mungu [101]
hawezi kusikia maombi yetu; lakini mwenye kutubia kosa lake, maombi yake yanakubaliwa mara moja. Hatuwezi sisi kujistahilisha machoni pa Mungu kwa matendo yetu mema; ustahilifu wa Yesu ndio utakaotuokoa, na damu yake ndiyo itakayotutakasa; hata hivyo kuna masharti juu yetu pia ili tukubaliwe na Mungu.

Sharti jingine juu yetu ni kuwa na imani. "Pasipo imani haiwezekani kumpendeza (Mungu): kwa maana mtu ampendezaye Mungu lazima aamini kwamba yuko, na kwamba huwapa thawabu wale wamtafutao." Waeb. 11:6. Yesu aliwaambia wanafunzi wake, "Yo yote myaombayo mkisali, aminini ya kwamba mnayapokea, nayo yatakuwa yenu." Marko 11:24. Je, twayasadiki maneno yake?

Kama tunakosa kupata mambo yale yale tuliyoyaomba, kwa wakati ule ule tuombao, hata hivyo tukubali ya kwamba Mungu hutusikia, tena atatujibu maombi yetu. Kwa ajili ya ujinga wetu, pengine twamwuliza Mungu mambo yasiyotufaa, naye Baba yetu wa mbinguni hutujibu na kutupa mambo yale yanayokuwa bora kwetu,—ambayo sisi wenyewe tungeyataka kama tungeweza kuona mambo yote jinsi yalivyo kama Mungu aonavyo. Hata kama inaonekana kwamba maombi yetu hayajibiwi, tutazidi kuendelea
[102] kutumaini ahadi yake; kwa kuwa bila shaka atatujibu baadaye, nasi, tutapata mbaraka ule ule unaotupasa. Lakini kusema ya kwamba Mungu hana budi kutujibu maombi tunayoomba na kutupa sisi yale yale tunayoyataka,—ni kama kujidai bila haki na kumfanyia Mungu kiburi. Mungu ni mwenye busara asiyeweza kufanya kosa, tena yu mwema; kwa hivyo hawanyimi waaminifu wake jambo jema lo lote. Ni heri tutegemee ahadi yake ya kweli, "Ombeni na mtapewa."

Tunapomwendea Mungu na kumwomba msamaha na mbaraka wake, imetupasa kuwa na moyo wa upendo na kusamehe wengine. Twawezaje kuomba hivi, "Utusamehe makosa yetu, kama sisi tunavyowasamehe waliotukosea." Na sisi katika roho zetu tungali hatujakubali kuwasamehe wengine? Tukitumaini kujibiwa maombi yetu, sharti tuwe na roho ya kuwasamehe wengine kama vile sisi tunavyotarajia kusamehewa.

Kudumu katika kuomba ni sharti jingine juu ya kujibiwa maombi. Kama tunataka kuongeza imani na kuwa watu wazima katika Kristo, imetupasa kuomba siku zote; "katika kusali, mkidumu;" "dumuni sana katika kuomba, mkikesha katika kuomba huku na shukrani." Warumi 12:12; Wakol. 4:2. Petro awausia Wakristo, "Mwe na akili, mkakeshe katika sala." 1 Petro 4:7. Mtume
[103] Paulo awaagiza hivi, "Katika kila neno kwa kusali na kuomba pamoja na kushukuru, haja zenu zijulike kwa Mungu." Wafil. 4:6. Na Yuda pia asema, "Ninyi, wapenzi, mkijijenga juu ya imani yenu iliyo takatifu, na kuomba katika Roho Mtakatifu, jilindeni katika upendo wa Mungu." Yuda 20, 21. Tukidumu katika kuomba, roho zetu zitafungamana kuwa moja na Mungu, ili tupate uzima utokao kwake; na maisha yetu yatakuwa safi machoni pake.

Sharti tufanye bidii katika kuomba; tusikubali kitu cho chote kutuzuia kuomba. Shika kila nafasi ya kwenda mahali ambapo watu huzoea kuomba. Wale watakao kushirikiana na Mungu kweli,

wataonekana kila mara kwenye mkutano wa kusali; watakuwa waaminifu katika kufanya iliyo wajibu wao, pia watakaza mioyo yao kupata msaada wote wa Mungu unaowahusu.

Sharti tuombe pamoja na watu wa nyumbani; na zaidi ya yote tusiwe wavivu katika kuomba faraghani peke yetu, maana kufanya hivyo ndio asili ya uzima wa roho. Kusali hadhara ya watu peke yake hakutoshi. Yatupasa kumfunulia Mungu mioyo yetu katika faragha, ambapo maombi yetu yatasikiwa na Mungu bila shaka; maana hapo tuna nafasi kumwonyesha mambo yetu yote. Katika sala ya upweke roho zetu hupata nguvu ya kustahimili katika kushindana na Shetani. Mungu ndiye nguvu zetu.

Omba faraghani; tena katika kufanya kazi yako, umwinulie [104]
Mungu moyo wako. Hivyo ndivyo Enok alivyopata kuendelea pamoja na Mungu. Shetani hawezi kamwe kumshinda yule ambaye moyo wake humtegemea Mungu hivi.

Hakuna wakati wala mahali pasipofaa kumwombea Mungu. Hakuna kinachoweza kutuzuia tusimwinulie mioyo yetu katika kusali. Kati ya watu njiani, hata katika kufanya kazi yetu, twaweza kumwomba Mungu msaada wake na uongozi wake, kama alivyofanya Nehemia alipomtolea mfalme Artashashta haja yake. Ni heri tumkaribishe Yesu aje akae mioyoni mwetu daima. Wale ambao mioyo yao i wazi kwa kupata msaada na mbaraka wa Mungu, hao wamo ulimwenguni kweli, lakini si watu wa ulimwengu kwa sababu hawapendi kufuata mambo na anasa za dunia. Hao nao hupatana na mambo ya mbinguni na kushirikiana na Mungu.

Mwonyeshe Mungu mahitaji yako, furaha yako, uzito wako, mashaka yako na hofu zako. Huwezi kumwudhi Mungu wala kumchosha. Yeye ambaye huhesabu nywele za kichwa chako, hawezi kuwa na kutojali kwa mahitaji ya watoto wake. "Bwana ni mwenye rehema nyingi, mwenye huruma." Yak. 5:11. Moyo wake wa upendo huingiwa na huruma kwa ajili ya huzuni na uzito wetu. Mwambie mambo yote yanayofadhaisha moyo. Hakuna [105]
msiba uwezao kumpata hata mtoto wake aliye mdogo, wala jambo linalomhangaisha au kumfurahisha, wala hakuna maombi yatokayo moyoni mwa mmojawapo wa watu wake, bila Baba yetu aliye mbinguni kuyaona yote na kusikia mara moja. Huyaangalia na kuyajali mambo yote yanayohusika na watu wake. "Huwaponya waliopondeka moyo, huziganga jeraha zao." Zab. 147:3. Mungu humfikiria

na kumwangalia kila mtu kana kwamba hakuna mtu mwingine wa kumshughulikia ila yeye tu ambaye Mwana wake Mpendwa alikufa kwa ajili yake.

Yesu alisema, "Mtaomba kwa jina langu: wala siwaambii ya kwamba mimi nitawaombea Baba: kwa maana Baba mwenyewe awapenda ninyi." Yoh. 16:26, 27. "Mimi niliyewachagua ninyi, . . . ili lo lote mmwombalo Baba kwa jina langu, awapeni." Yoh. 15:16. Na kuomba kwa jina la Yesu, maana yake siyo kulitaja tu jina lake katika mwanzo na mwisho wa sala. Maana yake ni hivi: katika kuomba kwetu tuwe na nia na roho ndani yetu iliyokuwamo ndani ya Yesu na kuziamini ahadi zake, kutegemea neema yake, na kutenda matendo ya namna yake.

Maisha yetu lazima kufanana na maisha ya Kristo, kwa kuomba na kufanya kazi pia. Yeye aombaye tu kila mara bila kufanya kazi
[106] yo yote, hatimaye maombi yake yatakuwa yasiyo na maana. Wale wasiomtumikia Yesu aliyewatumikia wao sana, hawana mambo yafaayo kuombwa, wala hawana sababu ya kusali. Watu kama hao hujifikiria nafsi zao wenyewe tu. Hawawezi kuwaombea wengine na kufikiri mahitaji yao, wala kuendesha ufalme wa Kristo na kupata nguvu za kumtendea kazi yake ya Injili.

Tunaona hasara tukikosa kushirikiana kwa kuimarishiana katika kumtumikia Mungu. Katika kushirikiana na kuongea kwetu sisi Wakristo twapata upungufu mkuwa sana kwa ajili ya kutokuwa na huruma sisi kwa sisi kama inavyotupasa. Lakini tukiandamana na watu na kufanya urafiki wa kweli nao, na kujua mambo yao, tunapata kuwahurumia wengine katika haja zao na misiba yao; pia ni njia ya kusitawisha mambo ya kiroho na kupata nguvu sisi wenyewe kwa kumtumikia Mungu.

Kama Wakristo wangekuwa wanashirikiana sawa sawa, na kuongea juu ya upendo wa Mungu na mambo yanayohusiana na ukombozi, mioyo yao wenyewe ingeburundika, pia wangewaburudisha wengine mioyo yao. Kama tungezidi kumfikiria Yesu na kuongea juu yake, na kutojifikiria sana nafsi zetu, Yesu angezidi kuwapo pamoja nasi.

[107] Kama tungemwaza Mungu kila mara kama vile Mungu anavyotuonyesha uangalifu wake kwetu, angekuwa katika fikara zetu milele. Twazoea kuongea juu ya mambo ya dunia hii kwa kuwa tunahusika nayo na kupendezwa nayo. Twaongea juu ya rafiki zetu

kwa sababu twawapenda. Tunafikiri sana juu ya mambo ya maisha ya kila siku, kama ni ya furaha au ya huzuni. Lakini imekuwa wajibu wetu kumpenda Mungu zaidi, kwa kuwa ametufanyia mema mno; ingefaa kuwa desturi na kawaida yetu kumfikiria Mungu zaidi ya wengine wote, na kuongea juu ya wema wake na uwezo wake.

Ni wajibu wetu kumshukuru Mungu zaidi kwa ajili ya "rehema zake na miujiza yake kwa wanadamu." Zab. 107:8. Asili ya kumwabudu Mungu si kutaka na kupata mahitaji yetu hasa. Tusifikiri juu ya haja zetu tu, bila kufikiri mibaraka tunayoipata. Sisi hatuombi zaidi kupita kiasi, lakini tunakosa kumtolea Mungu shukrani kwa kiasi kipasacho. Twapata rehema zake daima, walakini tunamshukuru kwa machache tu katika yote ambayo ametutendea.

Katika siku za zamani, Waisraeli walipokutanika katika mkutano wa dini, Mungu aliwaagiza hivi: "Ndipo mtakapokula mbele ya Bwana Mungu wenu, nanyi mtafurahia kila mtakazotia mikono,
ninyi na nyumba zenu, alizokubarikia Bwana Mungu wako." Kumbu. [108]
12: 7. Yote yatendwayo kwa kumtukuza Mungu yafaa kutendwa kwa furaha, na shangwe, na shukrani, siyo kwa huzuni na moyo mzito.

Mungu wetu ndiye Baba mwenye huruma na rehema. Imewapasa watu wake kumfurahia katika kumwabudu na kumtumikia. Yeye ambaye amewawekea watoto wake wokovu mkuu, hataki wamtumikie kama vile angalitaka msimamizi wa watumwa aliye mkali, na asiye na huruma. Mungu ndiye rafiki yao aliye bora zaidi; na wanapomwabudu naye hutumaini kuwa pamoja nao, kusudi awabariki na kuwafariji, akijaza mioyo yao furaha na upendo. Mungu ataka watoto wake waburudike moyo katika huduma yake, tena wasione kazi yake kuwa ni ngumu sana, bali wapate kupendezewa katika kumtumikia. Hata na wale wanaokutanika kumwabudu, Mungu hutaka wapate kufikiri juu ya uangalifu na upendo wake, ili wachangamshwe moyo katika mambo yote ya maisha yao, na kufanya yote kwa haki na uaminifu.

Kristo naye amesulubiwa, na hili ni jambo la kufikiriwa sana, lipasalo kuwa jambo kubwa katika maongezi yetu. Imetupasa kukumbuka mibaraka yote tunayoipata mkononi mwa Mungu; na kama tunafahamu upendo wake mkubwa usio na kifani, basi tukubali
kumwekea amana mambo yetu yote, yule aliyesulubiwa kwa ajili [109]
yetu.

Huko mbinguni Mungu husujudiwa kwa nyimbo na shangwe. Nasi tunapomtolea Mungu shukrani yetu, tunamtukuza kama vile anavyotukuzwa na majeshi ya mbinguni. “Atoaye za kushukuru, ndiye anitukuzaye.” Zab. 50:23. Hivyo tufike mbele zake “kwa zaburi na tenzi na nyimbo za roho, mkiimba na kumshangilia Bwana mioyoni mwenu; mkimshukuru Mungu Baba siku zote kwa mambo yote.” Soma Isa. 51:3; Waef 5:19.

Tafuta daima utakatifu;
Fanya urafiki na Wakristo tu;
Nena siku zote na Bwana wako:
Baraka uombe kwa kila jambo.

Tafuta daima utakatifu;
Uwe peke yako ukimwabudu;
Ukimwangalia Mwokozi wako,
Utabadilishwa kama alivyo.

Tafuta daima utakatifu;
Kiongozi wako awe Yesu tu;
Katika furaha au huzuni
Dumu kumafuata Yesu Mwokozi.

Tafuta daima utakatifu;
Umtawaze Roho moyoni mwako;
Akikuongoza katika haki,
Hufanywa tayari kwa kazi yake.

## Sura 12—Yatupasayo Kufanya Tukiwa na Mashaka Moyoni [110]

WATU wengi, hasa walio Wakristo wapya, siku zingine huwa na mashaka moyoni juu ya mambo mengine katika Biblia ambayo hawawezi kuyaeleza ama kuyafahamu. Naye Shetani huyatumia mambo yale kwa kuwapunguzia imani yao katika kukubali kwamba Biblia ni ufunuo wa Mungu. Wanasema, "Nawezaje kujua njia iliyo ya haki? Kama kweli Biblia ni Neno la Mungu, nawezaje kuondolewa mashaka haya moyoni, nisije nikashikwa na fadhaa?"

Kila jambo atakalo Mungu tulisadiki, hakosi kutubainishia sababu ya kuwa na imani juu ya jambo lile. Jinsi Mungu mwenyewe alivyo hai, namna ya tabia zake, na ukweli wa Neno lake, mambo haya yote yamehakikishwa kwetu kwa namna nyingi. Hata hivyo Mungu haoni ni afadhali kutuondolea nafasi ya kuwa na shaka. Imetupasa kumwamini Mungu kwa vile tunavyobainishiwa mioyoni mwetu juu ya mambo yasiyoonekana, siyo kwa ajili ya mambo yaliyo dhahiri katika macho yetu ya kibinadamu.

Haiyamkiniki kwa nia ya kibinadamu kufahamu kabisa namna [111] ya tabia za Mungu wala kazi yake. "Kwa kutafuta utampata Mungu? Utampata Mwenyiezi Mungu alivyo bora? Juu kama mbingu; utafanyaje? Chini kupita ahera; utajuaje?" Ayub 11:7, 8.

Mtume Paulo alisema, "Ee ajabu ya utajiri na hekima na maarifa ya Mungu; hazina hata kiasi! hukumu zake hazichunguziki, na njia zake hazitafutikani!" Warumi 11:33. Na hata "mawingu na giza yamemzunguka," "haki na hukumu maweko ya kiti chake." Zab. 97:2. Katika matendo yake juu yetu twaweza kufahamu makusudi yake kwa kutosha kuona upendo wake na huruma yake isiyo na kiasi, na jinsi uwezo wake ulivyo mkuu kupita cheo. Twaweza kutambua makusudi yake kwa kadiri inavyotufaa; zaidi ya hayo imetulazimu kumtawakali Mwenyiezi Mungu, ambaye moyo wake umejaa upendo.

Katika Neno la Mungu, vile vile katika sifa yake, kuna mambo ya siri wasiyoweza wanadamu kuyafahamu. Jinsi dhambi ilivyoingia

ulimwenguni, jinsi Kristo alivyojifanya kuwa na umbo halisi la binadamu, uzazi wa pili jinsi ulivyo, ufufuo, na mengineyo katika Biblia, ni mafumbo makubwa sana kushinda akili za kibinadamu kuyaeleza, wala kufahamu maana yake vizuri. Lakini hatuna sababu
[112] ya kuwa na shaka juu ya Neno la Mungu kwa ajili ya kutofahamu mafumbo ya uongozi wake na majaliwa yake. Hata katika mambo ya ulimwengu na viumbe vyake twaona mafumbo mengi tusiyoweza kuyafahamu. Wenye akili sana wameshindwa kueleza habari za uhai jinsi ulivyo, hata uhai wa vidudu vidogo. M.ahali pote pana maajabu tusiyoweza kuyafahamu. Kwa hivyo mbona tunastaajabu tukiambia kuwa kuna mambo ya kiroho yasiyowaza kufahamiwa na kuelezwa na binadamu? Shinda imekuwa kwa ajili ya udhaifu na akili chache za binadamu. Katika Maandiko yenyewe Mungu ametuhakikishia jinsi Maandiko haya yalivyo yake, tusione shaka moyoni juu ya Neno lake kwa sababu ya kutofahamu mafumbo yake yote.

Mtume Petro amesema kwamba katika Maandiko "yamo mambo ambayo ni vigumu kuelewa nayo; na mambo hayo watu wasio na elimu, wasio imara, huyapotoa . . . kwa upotevu wao wenyewe." 2 Pet. 3:16. Wengine husema ya kwamba mafumbo ya Biblia ni sababu ya kutosadiki maneno yake: lakini kwa kweli mafumbo haya ni ushahidi mkuu kuwa yametoka kwa Mungu. Kama ingekuwa Biblia haina habari za Mungu ila tu mambo yawezavo kuelezwa kwa urahisi na kufahamiwa na binadamu, Biblia isingekuwa na hakika kwamba ni ya Mungu kweli.

[113] Mafundisho ya Biblia juu ya wokovu, yametolewa kwa namna ifaayo kwa mahitaji na matakwa ya moyo wa binadamu; watu wastaarabu na wenye elimu nyingi wamevutwa na uzuri wa maneno yake; na hata watu duni waweza kuelewa na kufahamu njia ya wokovu. Hata hivyo twaweza kuyasadiki hivi tu, kwa kuwa Mungu ndiye anayetujulisha mambo hayo. Mpango wa Mungu juu ya ukombozi wa wanadamu umebainishwa vizuri kwetu, ili mtu ye yote ajue la kufanya katika kutubu kwa Mungu, na kuwa na imani kwa Bwana wetu Yesu Kristo, ili apate kuokoka kwa njia aliyoiweka Mungu. Walakini ndani ya mambo haya kuna mafumbo ya Mungu yasiyofunuliwa ila kwa yule anayeyachunguza kwa moyo na bidii. Na kwa jinsi anavyozidi kuyachunguza maneno ya Biblia, ndivyo anavyozidi kusadikishwa kwamba ni Neno la Mungu aliye hai.

Wenye kumkana Mungu hutupilia mbali Neno lake kwa sababu hawawezi kufahamu mafumbo yake yote. Hata na wengine wanaojidai kuwa wanasadiki Biblia, huona mashaka moyoni juu ya jambo hilo. Mtume amesema, "Angalieni, ndugu zangu, usiwe katika mmoja wenu moyo mbovu wa kutokuamini, kwa kujitenga na Mungu aliye hai. Waeb. 3:12. Ni vizuri kujifunza mafundisho ya Biblia, na kuchunguza "hata mafumbo ya Mungu," (1 Wakor. 2:10 ), kwa kadiri yana- vyofunuliwa katika Maandiko. Ingawa [114]
ni "kwa Bwana Mungu wetu yaliyo ya siri," ni kwetu sisi "yaliyofunuliwa," Kumbu. 29:29. Lakini ni kusudi la Shetani kuipotoa njia ya binadamu kama anataka kuyachunguza mambo. Kwa ajili ya ufundi wanaojiona kuwa nao katika kuchunguza mafundisho ya Biblia, watu wengine huwa wepesi wa kuchukizwa wasipoweza kueleza maana ya kila sehemu ya Maandiko kwa namna ya kutosheleza nafsi zao wenyewe. Ni aibu kwao kukiri ya kwamba hawayafahamu vizuri. Hawataki kumngojea Mungu hata atakapowafunulia maana ya hakika. Huona kwamba akili za kibinadamu zimetosha kuwafahamisha Maneno ya Mungu; nao wakishindwa kufanya hivi, basi huyakana kuwa si ya Mungu. Kuna maelezo na mafundisho mengi ya dini yanayodhaniwa tu ya kuwa asili yake ni maneno ya Biblia, lakini maana yake ni kinyume cha ukweli wa Biblia. Kwa ajili ya mambo hayo watu wengi hushikwa na fadhaa na kuona shaka mioyoni mwao. Lakin imekuwa hivyo si kwa ajili ya Neno la Mungu hasa, ila kwa kuwa wanadamu wamepotoa maneno yake.

Kama wanadamu wangeweza kupata kufahamu jinsi Mungu alivyo hasa, pamoja na matendo yake, basi, wasingekuwa na jambo jipya la kuvumbua, wasingezidi kuelimishwa tena, wasingepata kuzidisha maendeleo yao ya kiroho. Hapo Mungu asingekuwa [115]
Mwenye enzi; tena kwa vile ambavyo binadamu angekuwa amefika mwisho wa elimu na maarifa yote, asingepata maendeleo yo yote tena. Tumshukuru Mungu kwa kuwa si hivyo. Mungu ni mewnye uwezo wote, mwenye kujua yote; "ndani yake zimo hazina zote za hekima na maarifa." Wakol. 2:3. Maisha ya milele wanadamu watakuwa wanachunguza na kuendelea kufahamu akili za Mungu, wema wake, na enzi yake, bila mwisho.

Kuna njia moja tu kwa kupata kuelimishwa na kuendelea kufahamu Neno la Mungu,— kama Roho ya Mungu inang'aa mioyoni mwetu na kutumuliki. "Mambo ya Mungu hakuna ayajuaye ila

Roho ya Mungu;" "maana Roho huyachunguza yote, hata mafumbo ya Mungu." 1 Wakor. 2:11,10. Tena Mwokozi aliwaahidia wafuasi wake hivi: "Ajapo yeye, Roho ya kweli, atawaongozeni katika yote iliyo kweli; . . . atatwaa katika iliyo yangu, atawapasheni habari." Yoh. 16:13, 14.

Mungu ataka binadamu atumie akili zake. Kuchunguza na kujifunza Biblia kunaimarisha roho zetu kwa jinsi isivyowezekana katika kujifunza mambo yo yote mengine. Ili tupate Kufahamu Maandiko, na mioyo yetu isifadhaisnwe, imetupasa kuwa na imani na moyo mmoja kama watoto, tuwe tayari kufundishwa ua kum-
[116] womba Roho Mtakatifu msaada wake. Tukiona uwezo wa Mungu na akili zake jinsi vilivyo kuu zaidi pasipo kiasi, na kuelewa hali yetu ya kutoweza kufahamu namna ya utukufu wake, hapo basi imetupasa kunyenyekea; na tunapofunua katabu cha Neno lake, imetupasa kuwa na heshima na unyenyekevu moyoni kama tupo mbele yake hasa.

Kuna mambo mengi ya fumbo, ambayo Mungu atawadhihirishia wale watakao kweli kuyafahamu. Lakini bila uongozi wa Roho Mtakatifu binadamu huelekea kupotoa maneno ya Biblia na kueleza maana isiyo ya kweli. Masomo mengi ya wanadamu katika Biblia yamekuwa bure bila faida. Kama kitabu cha Neno la Mungu kinafunuliwa bila heshima na maombi: mtu asipomkazia Mungu fikara zake na upendo wake na kufanya mapenzi ya Mungu, bila shaka atashikwa na fadhaa. Ndipo Shetani atayatawala mawazo yake, na kumtilia moyoni mwake maelezo ya Biblia ya yasiyo ya kweli. Kila mara wanadamu wasipopatana na Mungu katika maneno na matendo yao, ingawa ni wenye maarifa ya namna gani, bila shaka watakosa kufahamu Maandiko, tena haifai kuyaamini maelezo yao. Wengi wao walio na mashaka moyoni, asili ya kushuku kwao ni kupenda dhambi. Masharti na vizuizi vya Neno la Mungu havipendezi wenye moyo wa kujisifu; na wale wasiokubali kufanya matakwa
[117] ya Biblia yake huwa wepesi kutosadiki kuwa ni Neno la Mungu halisi. Bali, wote watakao kwa moyo kujua matakwa ya Mungu na huyafanya, hao nao watabainishiwa kuwa Biblia na Maneno ya Mungu yawezayo kuwapa hekima hata wapate wokovu.

Kristo asema, "Mtu akipenda kuyatenda mapenzi yake, atajua habari ya elimu hii kwamba yatoka kwa Mungu." Yoh. 7:17. Badala ya kubishana bure juu ya mambo msiyoweza kuyafahamu, ni

heri mfanye kila wajibu wenu kwa vile mnavyofahamu na kuelewa nao, ndipo mtasaidiwa kuyafahamu na kuyafanya yale ambayo sasa mnayaonea mashaka.

Mungu ataka tujihakikishie ukweli wa Neno lake na ahadi zake. Asema, "Onjeni mwone BWANA ndiye mwema." Zab. 34:8. Tusitegemee neno la wengine, ila tuonje sisi wenyewe na kuona wema wake. Asema tena, "Ombeni, na mtapata," Yoh. 16:24. Ahadi zake zitatimia. Haziwezi kuwa na upungufu. Na kwa vile tunavyomkaribia Yesu, na kufurahishwa na upendo wake, ndivyo nuru yake itakavyong'aa mioyoni mwetu, tena mashaka na giza vitaondolewa. Mtume Paulo asema ya kwamba Mungu alituokoa "na nguvu za giza, akatuhamisha na kutuingiza katika ufalme wa Mwana wa pendo lake." Wakol. 1:13. Kila ambaye "amepita toka mauti hata uzima" anaweza kutia "muhuri wake kwamba Mungu ni wa kweli." Yoh. 5:24; 3: 33. Awe- za kushuhudia, "Nimepata msaada [118]
kwake Yesu; naye ameniruzuku mahitaji yangu yote, nimeshibishwa njaa ya moyo wangu; tena sasa Biblia inakuwa kwangu ufuno wa Yesu Kristo. Waniuliza mbona namwamini Yesu?—Kwa kuwa ni Mwokozi wangu. Kwa nini nasadiki Biblia? Kwa sababu nimeona kuwa ni sauti ya Mungu moyoni mwangu." Twaweza kuwa na ushuhuda ndani yetu kuwa neno la Biblia ni kweli, tena Kristo ni Mwana wa Mnngu. Twajua kwamba hatufuati hadithi zilizotungwa kwa werevu. 2 Petro 1:16.

Petro awaamuru Wakristo walio ndugu zake, "Kaeni katika neema, na katika kumjua Bwaua wetu, Mwokozi wetu Yesu Kristo." 2 Pet. 3:18. Watu wa Mungu wakikaa katika neema yake, watazidi kudhihirishiwa Neno lake. "Matembezi yao wenye haki kama nuru nyeupe, iangazayo ikizidi hata mchana utimiapo." Methali 4:18.

Kwa imani twaweza kutazama mbele hata mpaka ufalme wa Mungu, na kutumaini ahadi ya Mungu juu ya kutuzidisha akili, na jinsi uwezo wetu wote utakavyoungamana na uwezo wa Mungu. Twaweza kufurahi kwa kuwa yote ambayo sasa tumeshikwa na fadhaa nayo, hapo ndipo yatadhihirishwa kwetu; mambo yanayokuwa magumu kufahamiwa, wakati huo yataelezwa dhahiri. "Wakati wa sasa tunaona kwa kioo kwa jinsi ya fumbo; wakati ule uso kwa uso; [119]
wakati wa sasa nafahamu kwa sehemu; wakati ule nitajua sana jinsi ninavyojuliwa na mimi sana." 1 Wakor 13:12.

Kumtegemea Mwokozi,
    Kwangu tamu kabisa;
Kukubali Neno lake
    Nina raha moyoni.

    Kumtegemea Mwokozi,
Kwangu tamu kabisa;
    Kuamini damu yake
Nimeoshwa kamili.

Kumtegemea Mwokozi,
    Kwangu tamu kabisa;
Kwake daima napata
    Uzima na amani.

    Nafurahi kwa sababu
Nimekutegemea;
    Yesu, Mpendwa na Rafiki
Uwe nami dawamu.

## Sura 13—Kufurahia Mungu [120]

WATU wa Mungu wameitwa wajumbe wa Kristo, kwa kutangaza wema wa Bwana na rehema zake. Kwa vile Yesu alivyotudhihirishia sifa za Baba, hivyo na sisi imetupasa kuwadhihirishia wengine wasiomjua Kristo jinsi alivyo mwenye upendo, na mwenye huruma. Yesu alisema, "Kama ulivyonituma mimi ulimwenguni, nami vivyo hivyo naliwatuma wao ulimwenguni." Mimi ndani yao, na wewe ndani yangu,. . . . ili ulimwengu ujue ya kuwa ndiwe uliyenituma." Yoh. 17:18, 2, 3. Mtume Paulo huwaambia wanafunzi wa Yesu, Mnadhihirishwa kuwa ni barua ya Kristo," inavyojulikana "na kusomwa na watu wote." 2 Wakor. 3:3, 2. Kila mmoja wa watoto wake ni kama barua Yesu anayoipeleka ulimwenguni. Kama wewe ni mfuasi wa Kristo, u barua yake anayoipeleka kwa jamaa zako, mji wako na mtaa unaokaa. Yesu akaapo ndani yako, anataka kusema kwa mioyo yao wasiomjua. Pengine hawasomi Biblia na kusikia sauti yake humo; hawatambui upendo wa Mungu kwa kuumba kwake. Lakini kama wewe ni mjumbe wake wa kweli, pengine [121]
kwa sababu ya mwenendo wako mwema na matendo yako mema, wataongozwa wapate kujua kidogo wema wake ua kuvutwa kwake Yesu, hata kumpenda na kumtumikia.

Wakristo wamewekwa kuwaangazia wengine njia iendayo mbinguni; kuwaonyesha nuru itokayo kwa Kristo. Mienendo yao na sifa zao vyapasa kuwa safi, kuwajulisha wengine hakika ya Kristo na namna ya kumhudumia.

Nasi tukiwa wajumbe wa Kristo kweli tutakuwa watu wa furaha. Wakristo ambao huzoea kuwa na mioyo mizito, wagunao na kunung'unika, huonyesha wengine mfano usio wa kweli juu ya Mungu na maisha ya kikristo. Wale ambao mienendo yao na desturi zao zinafanya wengine kudhani kwamba Mungu hapendezwi kama watu wake wanafurahi, hao nao wanamshuhudia uwongo Baba yetu aliye mbinguni.

Shetani husimanga sana anapoweza kuwatilia watu wa Mungu fikara za kutoamini na kufa moyo. Hufurahi sana tukiona mashaka

mioyoni juu ya Mungu jinsi anavyotupenda na kuweza kutuokoa. Ni kazi ya Shetani kumtangazia Mungu kuwa hana huruma na rehema. Hujaribu kuutia moyo wa binadamu fikara za uwongo juu ya Mungu; nasi mara nyingi twasikiliza habari zile za uwongo, na ku-
[122] tomheshimu Mungu kwa ajili ya kutomwamini na kumnung'unikia. Shetani hujaribu kuwatia watu fikara kuwa njia ya kikristo ni ya taabu na shida. Tena Mkristo kama anaonyesha mashaka haya katika maisha yake, ni kama kusema yu pamoja na Shetani.

Wengi hufikiri sana juu ya makosa yao, upungufu wao na dhiki zao, hao nao mioyo yao hujaa huzuni na uchungu. Je, katika maisha yako hujapata mambo yafaayo kuyafurahia? Hata nyakati zingine hujaona furaha moyoni mwako kwa ajili ya mvuto na uongozi wa Roho ya Mungu? Hata hujaona uzuri wa ahadi za Mungu?

Kudumu kufikiri mambo haya yanayoutia moyo uchungu na kukata tamaa, ni kama kukusanya miiba na viwavi vinavyotuchoma na kutuuma, bila kuona maua na matunda jinsi yalivyo mazuri na ya kufurahisha moyo. Yule ambaye amekata tamaa, moyo wake umekufa ganzi, haoni nuru ya Mungu moyoni mwake, pia huwatia wengine giza njiani mwao.

Tumshukuru Mungu kwa vile ambavyo ametuhakikishia upendo wake kwa njia nyingi zitupasazo kuzifikiri mara kwa mara; Mwana wa Mungu jinsi alivyoacha utukufu wake, na kuwa katika mfano wa kibinadamu ili apate kutuokoa katika mamlaka ya Shetani; jinsi alivyomshinda Shetani, na kuinua binadamu toka katika hali ya uhal-
[123] ifu ambao aliuangukia kwa ajili ya dhambi, na kutupatanisha tena na Mungu; naye binadamu akivumilia na kustahimili hata mwisho kwa kumwamini Mwokozi, jinsi atakavyovikwa nguo nyeupe, yaani haki itokayo kwa Mungu, kwa imani—hayo ni mambo ambayo Mungu ataka tuyafikirie.

Ikionekana kwetu kana kwamba tuko katika hali ya kutosadiki upendo wa Mungu na ahadi zake, tunamdharau Mungu na kumhuzunisha Roho wake Mtakatifu. Mama fulani angeonaje kama watoto wake wangemnung'unikia mara kwa mara kama asiyetaka kuwatendea vizuri, naye hudumu kuwakifiri na kuwatendea mema? Na sisi je, Baba yetu aliye mbinguni ataonaje kama tunamdharau kwa upendo wake jinsi alivyomtoa Mwana wake wa pekee ili tupate uzima? Mtume Paulo alisema, "Yeye asiyemwachilia Mwana wake yeye, bali alimtoa kwa ajili yetu sisi, atakosaje kutukarimia na vitu vyote

pamoja naye?" Warumi 8:32. Hata hivyo kuna wengi ambao kwa matendo yao, si kwa maneno hasa, huwa wanasema, "Maneno haya ya Mungu hayanihusu mimi. Pengine awapenda wengine, lakini si mimi."

Katika kufanya hivyo unajihatarisha moyo wako mwenyewe; kwa kuwa kila mara unaposema maneno ya kushuku na kutoamini, unazidi kujithibitisha katika kutoamini; tena si wewe mwenyewe tu ambaye unajihatarisha kwa tendo hili; hata na wale ambao wanasikia maneno yako watavutwa kuwa na shaka pia, tena pengine haitawezekana kubatilisha matokeo ya maneno yako [124]
jinsi yatakavyokuwa mwishowe. Wewe mwenyewe labda utaweza kuokoka katika mtego wa udanganyifu wa Shetani, lakini wale waliovutwa nawe, pengine hawataweza kuondolewa mawazo yale uliyowatilia mioyoni mwao. Hivyo inatupasa sana kusema mambo yale tu yatakayozidisha nguvu na uzima wa kiroho!

Watu wote hupata majaribu: mambo ya kutia majonzi na huzuni, ambayo ni vigumu kuyastahimili; na mivuto ya Shetani, ambayo ni vigumu kuipinga. Tusiwasimulie wanadamu wenzetu taabu zetu na mambo ya kuwatilia mashaka mioyoni mwao; ila tumwonyeshe Mungu shida zetu zote katika sala zetu. Kwa namna ya maisha na maneno yetu, wengine waweza kutiwa moyo na kuzidishiwa nguvu, ama waweza kuingiliwa na mashaka na kuzuiliwa wasimtake Kristo na ukweli wake.

Ni kweli Mwokozi wetu alikuwa mtu wa huzuni, ajuaye taabu, kwa kuwa alichukua huzuni zote za wanadamu. Lakini ijapokuwa hivyo, moyo wake ulikuwa mtulivu, nao ulikuwa kama chemchemi ya uzima; po pote alipokwenda, aliwatilia watu raha, amani, furaha na shangwe mioyoni mwao. Alikuwa mtu wa moyo wa juhudi, asiye na chuki, wala mwenye uso mzito kamwe. Maisha yao wanaomfuata Mwokozi yatakuwa na kusudi jema; watafaha- mu jinsi walivyo na [125]
mzigo wa kuwa mfano wake mbele ya wengine. Hawatatoa ubishi na upuzi au kufanyiza mzaha, kwa kuwa dini ya Yesu ni yenye adibu na ya utaratibu: ni dini ya amani. Dini hii haizimi furaha wala kuzuia ukunjufu au vicheko vya upendo. Kristo hakuja kuhudumiwa bali kuhudumu; upendo wake ukiwamo moyoni tutafuata mfano wake.

Tukifikiri sana juu ya makosa ya wengine, ukali wao na matendo yao yasiyo na haki, haitawezekana kwetu kuwapenda jinsi Kristo

alivyotupenda sisi. I lakini tukifikiri zaidi juu ya pendo la ajabu na huruma ambayo Kristo anatuonyesha, haitakuwa vigumu kwetu kuonyesha roho ile ile kwa wengine. Tungependana na kuheshimiana ingawa tunajuana kuwa tunayo makosa. Tungejifunza kujidhili na kuwa na unyenyekevu na kuyavumilia makosa ya wengine kwa upole mwingi. Hivyo nia ya kujipendeza nafsi zetu itaondolewa na tutajawa na ukarimu wa moyo.

Mtunga Zaburi asema, "Umwamini Bwana, ukatende mema; ukae kwa nchi, ukaishike amini." Zab. 37:3. "Umwamini Bwana." Kila siku inaleta taabu na mahangaiko yake; nasi tu wepesi kuzungumza na wenzetu juu ya shida zetu na majaribu yetu, kana kwamba hatuna Mwokozi atupendaye, aliye mwepesi kusikia haja zetu zote, naye yu karibu sana kutusaidia katika shida.

[126] Wengine huzoea kuwa na hofu na kutazamia shida isiyokuwapo bado. Siku zote sisi huzungukwa na vitu vinavyoonyesha upendo wake; kila siku hufurahishwa na wingi wa majaliwa ya Mungu; lakini wengine wetu husahau mibaraka ya sasa hivi, na huzoea kufikiri mabaya wanayodhani labda yatakuja.

Je, imetupasa kutokuwa na shukrani na amini hivi? Yesu ndiye rafiki yetu. Wa mbinguni wote hutufikiri sisi. Tusife moyo; tumtwike Bwana taabu zetu zote, nasi tuwe na amani na uchangamfu. Tumwombe Mungu hekima na akili katika kufanya shughuli zetu, ili tusipate hasara na misiba. Yesu ameahidi msaada wake, lakini inatupasa pia tufanye juhudi sisi wenyewe. Mungu hapendi ili tutaabike. Bwana wetu hatudanganyi. Hasemi, "Msiogope; hamtapata kuhatarishwa kamwe." Si kusudi lake kuwatoa watu wake katika dunia palipo dhambi na maovu, lakini huwaonyesha mahali pa kukimbilia kwa kupata msaada. Aliwaombea wafuasi wake hivi: "Siombi uwatoe katika ulimwengu, bali uwalinde na yule mwovu." Alisema pia' "Ulimwenguni mtapata shida: lakini jipeni moyo: mimi nimeushinda ulimwengu." Yoh. 17:15; 16:33.

Katika mafundisho yake mlimani, Kristo aliwafundisha wafuasi wake kwamba ni lazima kumtumaini Mungu. Mafundisho haya yali-
[127] kusudiwa kusaidia watu wa Mungu siku zote hata siku hizi ili wajipe moyo. Mwokozi aliwaonyesha ndege za anga, jinsi waimbavyo bila kufadhaika moyo; "hawapandi, wala hawavuni." Lakini Baba aliye mbinguni awalisha. Ndipo Mwokozi anauliza, "Ninyi je! si bora kupita hao?" Mattayo 6:26. Baba mkuu hufunua mkono

wake, huviruzuku viumbe vyake vyote mahitaji yao. Ndege hawana budi kudonoa punje za nafaka na vitu vinginevyo vinavyokuwa chakula chao. Imekuwa juu yao kuokota vitu vya kutengeneza viota vyao. Wamelazimishwa kuwalisha watoto wao. Hao nao huondoka kufanya kazi yao na wimbo kwa kuwa "Baba yenu wa mbinguni awalisha hao." Na "ninyi je! si bora kupita hao?" Naye alituumba sisi katika mfano wake mwenyewe, naye angekosa kuturuzuku mahitaji yetu kama tunamtumainia?

Kristo alielekeza nia za wafuasi wake kwa maua ya mashamba, jinsi yameavyo. Alisema kwamba "hata Sulemani katika utukufu wake wote hakuvikwa kama moja la hayo." Naye Yesu auliza, "Lakini Mungu akiyavika hivi majani ya mashamba, yaliyopo leo, na kesho hutupwa kalibuni, je, hatazidi sana kuwavika ninyi, enyi wa imani haba?" Mattayo 6:28, 30. Fundisho hili la Kristo linakaripia masumbufu na mahangaiko ya moyo usio na amani.

Mungu ataka watu wake wote wawe na moyo wa furaha na [128]
utulivu, na usikivu. Yesu alisema, "Amani nawaachieni; amani yangu nawatolea; si kama ulimwengu utoavyo, mimi nawatolea. Msifadhaike mioyo yenu, wala msiwe na woga." "Haya nimewaambieni, ili furaha yangu iwe ndani yenu, na furaha yenu itimizwe." Yoh. 14:27; 15:11.

Furaha inayotakiwa na mtu fulani kwa ajili ya kujipendeza mwenyewe tu, bila kufanya yanayompasa, hiyo ndiyo furaha isiyofaa, isiyo na faida, furaha isiyodumu. Lakini katika kumhudumia Mungu, Mkristo aweza kupata furaha na kuridhishwa moyo. Ingawa tunakosa anasa za maisha haya, twaweza kuona furaha moyoni katika kutumainia maisha yajayo ya milele.

Lakini hata hapa duniani Wakristo waweza kufurahi katika kumshiriki Kristo na kuongea naye; waweza kujua upendo wake, na kufarijiwa moyoni. Kila siku katika maisha haya ya sasa twaweza kuzidi kumkaribia Yesu na kuzidi kujua upendo wake jinsi ulivyo kwetu. Tusiutupe ujasiri wetu; bali tushikamane sana "na ujasiri wetu, . . . kwa kutumaini mpaka mwisho." Waeb. 10:35; 3:6. "Hata sasa Bwana ametusaidia," pia atatusaidia mpaka mwisho. Ni heri tudumu kufikiri mambo yaliyo ukumbusho kwetu, jinsi Bwana alivyotusaidia na kutuokoa mkononi mwake aliye mharabu. Tuki-
zoea kukumbuka jinsi Mungu alivyotuhurumia—machozi ambayo [129]
ameyafuta katika macho yetu, maumivu yetu aliyovatuliza, jinsi

alivyotuondolea fadhaa na hofu mioyoni mwetu, jinsi alivyoturuzuku mahitaji yetu, na mibaraka yake ambayo tumeipata— tutajipa moyo kwa kujiweza kustahimili yote yatakayotupata katika siku zijazo.

Katika mashindano ya yule mwovu yatakayokuwa kwa siku zijazo, twajua ya kwamba tutafadhaika moyoni; lakini kwa vile tunavyofikiri mambo yaliyopita na kusema, "Hata sasa Bwana ametusaidia," twaweza kutazamia mambo yatakayokuja na kujua hivi: "Na kadiri ya siku kadhalika nguvu zako." 1 Sam. 7:12; Kumbu. 33:25. Majaribu hayatakuwa makali kushinda nguvu tutakayopewa kuyastahimili. Kwa hiyo tushike kazi yetu jinsi ilivyo, na kutumaini kwamba tukipatwa na jambo lo lote, bila shaka tutapewa nguvu kwa kadiri ya jaribio lile ili tuweze kustahimili.

Hatimaye milango ya mbinguni itafunguliwa kuwakaribisha wana wa Mungu, naye Mfalme wa utukufu atawaambia, "Njooni, mliobarikiwa wa Baba yangu, urithini ufalme mliowekewa tangu kuumbwa ulimwengu." Mattayo 25:34.

Ndipo waliokorabolewa watakaribishwa hapo Yesu anapowaandalia. Hapo majirani zao hawatakuwa waovu wa dunia, waongo,
[130] makafiri, wasio na usafi na wenye kutoamini; bali watashirikiana nao waliomshinda Shetani, wenye kufanana na Mungu na kuwa na sifa kamili. Kila tamaa ya dhambi, kila ukosefu na hila ambavyo tunavyo katika hali yetu ya sasa, vitakuwa vimefutwa na damu ya Kristo; hao nao watapata uzuri usio na kiasi na kuwa na utukufu wa Kristo. Watakuwa na sifa kamilifu kwake; watasimama mbele ya "kiti cha enzi, cheupe, kikubwa," wakiwa hawana hila na mawaa.

Kwa sababu ya utukufu wa urithi uliowekwa kwake, "mtu atatoa nini badala ya roho yake?" Mattayo 16:26. Hata amekuwa maskini, mwana wa Mungu huwa na utajiri na heshima ambavyo haviwezi kupatikana kwa dunia. Moyo uliokombolewa na kusafishwa dhambi, na kujitoa kumtumikia Mungu, umekuwa wa thamani kubwa isiyokadiriwa; iko furaha mbele ya Mungu na malaika zake kwa mwenye dhambi mmoja atubuye, furaha inayoonyeshwa kwa nyimbo za shangwe.

Nitaonana na Yesu, uso kwa uso kweli;
    Siku ile shangwe tele nikimwona Mwokozi.
Tutaonana kwa macho, huko kwetu mbinguni;
    Na kwa utukufu wake nitamwona milele.

Sasa siwezi kujua jinsi alivyo hasa;
   Bali atakapokuja, nitamwona halisi.
Mbele yake yafukuzwa machozi na huzuni;
   Kipotovu kitanyoshwa, fumbo litafumbuka.
Uso kwa uso! Hakika palepale furaha;
   Nitafurahi kabisa nikimwona Mwokozi.